

Mtumiaji

Jarida la habari zenyet kuwajengea uelewa watumiaji wa huduma za Nishati na Maji



ISSN 2738-9014

Toleo Na. 09 • Januari- Juni, 2024

Baraza laendeleza uwakilishi kwa wananchi

■ Laelimisha watumiaji 58,770

HALIUZWI

- **Malalamiko 1,946 yatatuliwa kwa ufanisi**
 - 1,011 yanahuusu maji
 - 857 umeme
 - 66 Mafuta
 - 12 Gesi



Twen'zetu na Nishati Safi ya Kupikia



Kutoka Ofisi ya Katibu Mtendaji

Karibu kwenye toleo la 09 la Jarida la Mtumiaji! Kwa niaba ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), ninayo furaha kubwa kwa mara nyingine kukukaribisha msomaji na mdau wetu katika ulimwengu wa habari zenye kuelimisha umma kuhusu huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA.

Katika toleo hili tunakuletea habari muhimu kuhusu huduma za umeme, maji, mafuta, gesi na masuala yanayowahusu sekta tajwa.

Habari na Makala katika toleo hili zimeandalisha kwa weledi mkubwa, ikiwa ni matumaini yetu kuwa si tu utapata taarifa muhimu, bali pia elimu itakayokuwezesha kupata ufahamu/uelewa wa haki na wajibu wako, matumizi sahihi, salama na endelevu ya huduma za nishati na maji pamoja na masuala mengine yanayohusu sekta tajwa.

Aidha, kupitia Toleo hili la Jarida la Mtumiaji, utapata ufahamu wa namna gani Baraza limetekeleza majukumu yake na hivyo kuchangia katika maendeleo ya sekta za nishati na maji katika jamii ya Watanzania. Utakutana na habari na Makala za kusisimua zikiwemo shuhuda za watu waliosadiwa na Baraza kutatua malalamiko yao, bila kusahau elimu kuhusu sheria na kanuni zinazomlinda mtumiaji wa huduma za nishati na maji.

Ni matumaini yetu kuwa utafurahi kusoma na kuelimika kutokana na Habari na Makala zilizoandikwa kwa umakini.

Kwa mara nyingine nikukaribishe na kukutakia usomaji mzuri wa toleo hili.



Stella Lupimo
KAIMU KATIBU MTENDAJI

Baraza laendeleza uwakilishi kwa wananchi



Prof. Epaphra Mushi, Mjumbe wa Baraza akizungumza na vyombo vya habari wakati wa maonesho ya kitaifa ya Nanenane 2023 yaliyofanyika jijini Mbeya kwenye Viwanja vya Mwakangale. Picha na Mpigapicha Wetu

Na Lugiko L. Lugiko, Dodoma

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limeendelea kuiishi kwa vitendo kaulimbiu yake ya "Huduma Bora ni Haki Yako" inayoakisi kuwa, mtumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ana haki ya kisheria ya kupata huduma inayokidhi ubora unaokubalika.

Hayo yamebainishwa kupitia tarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Baraza kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba 2023 ambayo inaonesha kuwa, Baraza limefanya jitihada kubwa katika kuwafikia wananchi kwa kutoa elimu, kutatua malala-

miko ya watumiaji na kuwawakilisha vyema katika vyombo vya maamuzi mbalimbali vya Serikali.

Akizungumzia taarifa hiyo, Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza Bi. Stella Lupimo alisema kuwa Baraza limepiga hatua kubwa katika kipindi tajwa kwa kuhakikisha kuwa watumiaji wengi wanapata uwakilishi katika masuala yanayogusa huduma za nishati na maji katika maisha yao ya kila siku.

"Likiwa ni moja ya jukumu lake la kisheria, Baraza katika kipindi cha Julai mpaka Desemba 2023 limetoa uwakilishi na utetezi kwa watumiaji kwa namna mbalimbali. Kwa ujumla Baraza limefanikiwa kuwafikia na kuwapatia elimu watumiaji 58,770 kuhusu masuala mtambuka katika sekta za nishati na maji ikiwemo

haki na wajibu wa mtumiaji. Idadi hii imefikiwa kupitia jumla ya programu 204 za uelimishaji," alisema Bi. Lupimo.

Alisema kuwa "watu tuliofifikia ni kutoka makundi mbalimbali ya watumiaji wakiwemo walimu wa shule za msingi na sekondari, waandishi wa habari, makundi ya vijana, akina mama, wafanyakishara katika masoko, waendesha pikipiki maarufu "Bodaboda", madereva wa daladala na jamii kwa ujumla kupitia vipindi vya radio na mikutano ya hadhara."

Kwa upande wa utatuzi wa malalamiko na kero za wananchi kuhusu huduma za umeme, maji, mafuta na gesi za kupikia majumbani (LPG), Kaimu Katibu Mtendaji huyo alisema Baraza limekuwa likichukua

Inaendelea Uk. 4

kwa uzito utatuzi wa kero hizo za wananchi.

"Utatuzi wa kero za wananchi ni moja ya vipaumbele muhimu vya Baraza na katika kipindi hiki Baraza limepokea jumla ya malalamiko 1,946 kutoka kwa watumiaji ambapo kati ya malalamiko hayo, 1,011 yanahusu huduma za maji, 857 umeme, 66 mafuta, na 12 ni gesi ya LPG," alisema Bi. Lupimo na kuongeza kuwa kupitia utaratibu wa Baraza, malalamiko yote haya yamefanyiwa kazi na kutatuliwa kwa ufanisi.

Taarifa hiyo ya utekelezaji wa majukumu ya Baraza pia imebainisha kuwa kwa kipindi hicho, Baraza limeshiriki katika mikutano nane (08) ya kutoa maoni kuhusu mabadiliko ya bei za huduma yaani taftishi (public hearing meetings) ambapo Baraza lilishauri na kutoa maoni yake kuhusu maombi mbalimbali yaliyowasilishwa EWURA.

Akifafanua kuhusu mikutano hiyo, Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza alisema kuwa Baraza liliandaa maoni na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa EWURA na mamlaka za maji ili kuhakikisha kuwa huduma hizo zinakawa bora, endelevu, zinazofikika kwa wananchi na kwa gharama nafuu ambazo wananchi wanaweza kuzimudu.

Baraza laendeleza uwakilishi kwa wananchi

"Ikiwa ni moja ya jukumu lake la msingi, Baraza limeshiriki katika mikutano ya taftishi za Mamlaka mbalimbali za Majisafi na Usafi wa Mazingira zikiwemo za Mafinga, Igunga, Nzega, Vwawa, Busega, Shinyanga, Kigoma, pamoja na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Biharamulo," alisema Bi. Lupimo.

Bi. Lupimo alisema kuwa kazi hizo ni mafanikio makubwa kwa Baraza licha ya kuwa Baraza linatimiza majukumu yake ya kisheria lakini pia limejidhatiti kuwa msaada muhimu kwa watumiaji wa huduma za nishati na maji kwa maslahi mapana ya taifa.

"Unapokuwa na jamii ya watu wanatambua haki zao na kujua wajibu wao ikiwemo kulinda miundombinu ya huduma za umeme na maji inayotengenezwa na serikali kwa gharama kubwa unasaidia ukuaji wa uchumi wa mtu mmojammoja na taifa kwa ujumla, na hivyo EWURA CCC ina-

jivunia kuwa sehemu ya mafanikio haya muhimu kwa taifa," alisema Bi. Lupimo.


Taaarifa hiyo ya kazi ya Baraza imefafanua kuwa, Baraza limeongenza wigo wa kujitangaza miongoni mwa watumiaji nchini kwa kutumia majukwaa mbalimbali ikiwemo matumizi ya teknolojia na ushiriki katika maonesho makubwa ya kitaifa na kimataifa, lengo likiwa na kuhakikisha watumiaji wengi wanatambua uwepo wa Baraza na kuwafikia mahali waliko.

"Baraza limezidi kuongeza wigo katika kuwafikia wananchi na kujitangaza zaidi kwa kutumia tovuti yake na mitandao ya kijamii ikiwemo kurasa zake za Facebook, Instagram, X zamani ikiujulikana kama Twitter na hata kupitia ushiriki wake katika maonesho ya kimataifa ya Sabasaba na yale ya Nanenane," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Taarifa hiyo inaonesha pia kuwa Baraza limejipanga vyema kuwafikia watumiaji wengi zaidi katika kipindi kijacho cha Januari hadi Juni 2024, ikiwa ni pamoja na kupokea na kutatta malalamiko yao, kutoa elimu na kuwawakilisha watumiaji katika vyombo mbalimbali vya maamuzi ikiwemo mikutano ya taftishi.



Bi. Anna Mungai, akizungumza wakati wa ziara ya Baraza katika Ofisi za Bodii ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu mkoani Morogoro hivi karibuni. Picha na Mpigapicha Wetu



Jipange kutumia nishati safi ya kupikia

Kwa miaka mingi, Tanzania imekabiliana na changamoto za nishati, ambapo matumizi ya kuni na mkaa yamekuwa yakishamiri ikiwa ni wazi kwamba jambo hili lina matokeo mabaya kwa mazingira na afya zetu kwa ujumla.

Kutokana na nia njema ya serikali ya kutsunza mazingira na uhifadhi wa rasimili misitu, ni wakati muafaka sasa wa kuchukua hatua kuelekea matumizi ya nishati safi zaidi katika shughuli za kupikia. Kutumia nishati safi kwa ajili ya kupikia ni muhimu kwa maendeleo endeleu ya mtu binafsi na taifa kwa ujumla hasa katika mustakabili wa utunzaji mazingira.

Kwa uchache, manufaa muhimu kutokana na matumizi ya nishati hii ni kama inavyoainishwa hapa chini.

Mosi, afya ya jamii: Kwa kutumia nishati safi, tunaweza kuboresha afya ya jamii yetu na kupunguza hatari ya kupata athari zitokanazo na madhara ya kutumia mkaa au kuni kama vile madhara ya macho, kukoho, mafua n.k. Kulingana na taarifa zilizopo katika tovuti ya Shirika la Afya Duniani (WHO), matumizi ya kuni yana madhara yanayoweza kusababisha vifo vinavyotokana na matatizo ya mfumo wa kupumua yanayosababishwa na uchafuzi wa hewa.

Pili, uhifadhi wa mazingira: Kwa kutumia nishati safi kama vile gesi ya kupikia au nishati ya umeme, tunaweza kupunguza uharibifu kwenye misitu yetu na kujiepusha na hatari ya jangwa, na kuchangia katika uhifadhi wa mazingira. Ripoti ya Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS), "National Environment Statistics Report (NESR, 2017) Tanzania Mainland" inaonesha kuwa matumizi ya mkaa na kuni yanachangia uharibifu wa misitu nchini.

Tatu, kuongeza ufanisi katika kupika: Matumizi ya gesi au vifaa vya umeme, yanaweza kuwa na ufanisi zaidi katika matumizi. Hii inamaanisha kuwa, mbali na kuwa safi, tunaweza kupata thamani kubwa zaidi kwa kiasi kidogo cha nishati tunachotumia na kuokoa muda pia.

Ripoti ya mwaka 2020 ya Chama cha Nishati Mbadala Tanzania (Tanzania Renewable Energy Association (TAREA) inaonesha kuwa majiko yanayotumia nishati safi yanaweza kupunguza matumizi ya nishati kwa asilimia fulani ikilinganishwa na njia za jadi za kupikia.

Nne, kuchoea uchumi: Kukuza matumizi ya vifaa vya kupikia vinavyotumia nishati safi kunaweza kuchoea sekta ya nishati mbadala na kutoa fursa za ajira. Hili linawezekana kupitia uanzishwaji wa miradi ya kutengeneza vifaa vinavyotumia umeme au gesi kidogo, uzalishaji wa "bio gas" n.k. Hii inaweza kusaidia kupunguza tatizo la ajira na kukuza uchumi mionganoni mwa jamii.

Huu ni wakati kwa mashirika ya kiraia na wananchi kwa ujumla kufanya kazi kwa pamoma ili kufanikisha mabadiliko haya. Tunaamini kuwa kwa kuunga mkono jitihada za Serikali kupitia "DIRA YA TAIFA YA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA 2033" haya yanaweza kufanikiwa kwa kila mmoja kufanya sehemu yake.

Katika kuunga mkono jitihada za Serikali juu ya wananchi kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia, EWURA CCC imejipanga vyema na iko tayari kushiriki kikamilifu mpanago wa Serikali katika kutekeleza jambo hili kwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia.

EWURA CCC ina uzoefu wa zaidi ya miaka 16 katika kufanya uelimishaji na uhamasishaji kwa kuyakutanisha makundi mbalimbali ya wadau na kuyajengea uelewa wa huduma za nishati na maji pote Tanzania Bara ambapo hutumia njia mbalimbali kama vile redio za kijamii, kufikia wananchi masokoni, kwenye nyumba za ibada, kwenye taasisi za elimu n.k.

Shime wananchi, wakati umefika sasa tutipange kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia. Ni wajibu wetu kutoa mchango wetu kwa kizazi hiki na kuhakikisha kwamba tunaacha Tanzania bora kwa vizazi vijavyo kwa kutunza mazingira yetu.

BODI YA UHARIRI
Stella Lupimo
- Mwenyekiti/Mhariri Mkuu
Geofrey Sokesia - Mhariri Msanifu
Lugiko L. Lugiko - Mjumbe
Josephine Ntaumenya - Mjumbe
Zamda Mabada - Mjumbe
Emmanuel Paul - Mjumbe

Wachangaji
Chiwegwa Samwel
Anadoris Komba
Nuru Zuberi
Ramadhani Kakende
Sakina Yusuph
Wadi Omari
Neema Nnko
Dennis Ndau
Catherine Ochido
Noela Ntiluvakule
Magreth Temba
Brenda Magoma
Amani Mbogo

Mawasiliano
Baraza la Ushauri la Watumiaji
wa Huduma za Nishati na Maji
Jengo la PSSSF Kambarage Tower
Barabara ya Jakaya CCM
S.L.P. 772, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2960 099
Baruaapepe: info@ewuracc.go.tz
Tovuti: www.ewuracc.go.tz

 EwuraCCC



Bi. Mosi Salum Simba, mkazi wa mtaa wa Barabara ya Musoma, Nzega Mjini akitoa maoni wakati wa mukutano wa taftishi kujadili maombi ya bei mpya ya maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega (NZUWASA) mnamo Agosti 2023 uliofanyika mjini Nzega. Picha na Mpigapicha Wetu

Wanawake Nzega wapinga ongezeko bei ya maji

Na Sakina Yusuf, Tabora

Wanawake wa mji wa Nzega wamejitekeza kwa wingi na kupinga ongezeko la bei ya maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega (NZUWASA) wakati wa kikao cha taftishi kilichoandaliwa na Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kilichofanyika hivi karibuni kwa lengo la kupata maoni juu ya maombi ya NZUWASA ya kurekebisha bei za maji.

Wakiongea kwa hisia, wanawake hao walitoa maoni yao kwa kupinga ongezeko la bei lililoombwa na NZUWASA kwa kusema kuwa gharama hizo ni kubwa na hivyo itawa-fanya washindwe kumudu kwani imeongezeka kutoka TZS 1500 hadi kufikia TZS 2,610 kwa mwaka 2023/2024, TZS 2,891 kwa mwaka 2024/2025 na TZS 2,974 kwa mwaka 2025/2026 kiasi ambacho ni sawa na asilimia 74.

Akitoa maoni yake Bi. Mosi Salum Simba mkazi wa Barabara ya Musoma, Nzega aliiomba EWURA kutokubaliana na maombi ya bei mpya zilizopendekezwa na NZUWASA kwani bei iliyopo bado ni kubwa

na kuna wananchi wengine bado hawawezi kumudu gharama hizo.

"Bei ya sasa bado ni kubwa sana na wengi wetu hatuwezi kuimudu hivyo naomba mtusaidie bei isipande nasi tunufaikie na huduma ya maji," alisema Bi. Simba.

Naye Bi. Zawadi Suleiman Chamsambo alilalamikia ongezeko hilo kubwa kwenye gharama za kurejesha huduma kutoka kiasi cha shilingi 15,000 cha sasa mpaka kufikia kiasi cha shilingi 35,000.

"Mfano una deni la 15,000 uki-ktiwa maji na ukataka kurejesha huduma unatakiwa ulipe faini ya shilingi 35,000; sasa jiulize ikiwa nimeshindwa kulipa shilingi 15,000, je nitawenza kulipa hiyo shilingi 35,000?" alihoji Bi. Chamsambo.

Akiwasilisha maoni ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) Bi. Hawa Ng'humbi ambaye ni Mjumbe wa EWURA CCC alitoa ushauri mbadala kuepusha ongezeko la bei za huduma zilizoombwa na NZUWASA hasa kwenye kipengele cha gharama za kurejesha huduma huku akiishauri NZUWASA kutafuta vyanzo mbadala vya mapato ili kuepuka kuongeza bei kwa watumiaji.

"Baraza limepitia maombi hayo

ya mabadiliko ya bei zinazoombwa na NZUWASA na kujiridhisha kwamba ongezeko hilo ni kubwa kwa makundi yote ya watumiaji wa huduma hiyo na litawaathiri pakubwa watumiaji na kuleta taha-ruki. Baraza linaishauri NZUWASA kutafuta njia mbadala ya kuongeza mapato tofauti na kuongeza bei zikiwemo kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji mapato yake na kuwafungia wateja wote dira za kuliapia kabla ya matumizi (pre-paid meters) ili kumpunguzia mzigo mtumiaji," alisema Bi. Ng'umbi.

Aidha Bi. Ng'umbi alionesha kufurahishwa na ushiriki mzuri wa wananchi hususani akina mama katika taftishi hiyo, na kuwapongeza wanawake hao kwa jinsi walivoyitokeza kwa wingi ili kupaza sauti zao juu ya kadhia wanazozipata kwenye huduma za maji.

"Mbali na kutoa maoni ya Baraza naomba niwapongeze sana akina mama wa Nzega kwa kushiriki kwa wingi katika kikao hiki tofauti na maeneo mengine ambayo nilishawahi kuhudhuria mikutano ya namna hii. Wanawake tunatakiwa tuwe mstari wa mbele kuhakikisha tunashiriki kwenye mambo muhimu kama haya yanayoweza kuathiri au kuimarisha hali zetu za kiafya na kichumi," alisisitiza bi Ng'umbi.

Baraza la Ushauri la watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkao wa Tabora litaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kushiriki vikao vya taftishi hasa kwa wanawake ili kuongeza ushiriki na kuleta chachu ya mabadiliko katika sekta za nishati na maji kwa kuwa ushiriki wao katika mikutano kama hii ni wa muhimu sana.

Endelezeni kazi nzuri mnayoifanya - Mramba

Na Mwandishi Wetu, Ilala

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Felchesmi Mramba amelishauri Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kuendeleza jithada katika kutekeleza kazi nzuri wanayoifanya ya kuelimisha na kutetea watumiaji wa huduma za nishati na maji nchini.

Mha. Mramba, ametoa ushauri huo alipotembelea banda la EWURA CCC wakati wa maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Sabasaba yaliyofanya mkoani Dar es Salaam katika viwanja vya Mwl. J.K. Nyerere.

Mha. Mramba alisema "nawapongeza kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kumlinda na kumteea mtumiaji wa huduma za nishati na maji. Ninyi ni kiungo muhimu sana katika jamii kwa sababu mnaweweza kumfikia mtumiaji wa mwisho kabisa wa huduma hizi na pia mnawasadida watumiaji katika mambo mbalimbali yanayohusu huduma za nishati na

maji."

Pamoja na pongezi hizo Mha. Mramba alitaka kufahamu kama Baraza limejitanua kwa kuwa na ofisi kwenye mikoa mingine tofauti na Mkoa wa Dar es Salaam.

Akijibu swalii hilo Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala wa EWURA CCC mkao wa kikazi wa Ilala Bi. Catherine Charles alimueleza Katibu Mkuu huyo kuwa, hadi sasa Baraza limeshafungua ofisi katika mikoa 21 ya Tanzania Bara.

"Mbali na ofisi hizo pia tuna kamati za kimikoa zinazofahamika kama RCC (Regional Consumer Committees) ambazo zinatekeleza majukumu ya Baraza kwenye mikoa husika. Kamati hizo zipo kwenye mikoa yote ya Tanzania Bara kwa ajili ya kuwasifikia na kuwasaidia watumiaji wa huduma za nishati na maji."

Bi. Charles alimweleza Katibu Mkuu huyo kuwa katika kila mkao wenye ofisi kuna Afisa wa Baraza ambaye anasaidiana na Wajumbe wa Kamati hizo za mkao kutekeleza ma-

jurumu ya kulinda na kutetea masilahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji.

Alisema, katika maonesho hayo Baraza liliwafikia watumiaji 1,740 na kuwaelimisha kuhusu Baraza na kazi zake, haki na wajibu wa mtumiaji, utaratibu wa kuwasilisha na kushughulikia malalamiko, matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji pamoja na viwango vya ubora wa huduma za nishati na maji.

Aidha, kupitia maonesho hayo, jumla ya malalamiko 92 kutoka kwa wadau mbalimbali walitembelea banda hilo yalipokelewa ambapo baadhi yake yalipatiwa ufumbuzi hapo hapo na mengine kupelekwa kwa watoa huduma kwa ajili ya utatuzi wake.

EWURA CCC kupitia mkoaa wa kizazi wa Ilala, itaendelea na programu za elimu kwa umma kwa kuhakikisha fursa zote muhimu za utoaji elimu zinatumia ili kuwajengea uelewa watumiaji wa huduma za nishati na maji na hivyo kuwa na mchango kati-ka uboreshaji wa huduma hizo nchini.



Mha. Felchesmi Mramba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati (wa kwanza kushoto) akisikiliza kwa makini maelezo kuhusu Baraza na kazi zake kutoka kwa Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala EWURA CCC Ilala Bi. Catherine Charles, alipotembelea banda la Baraza wakati wa maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) jijini Dar es Salaam. Picha na Mpigapicha Wetu

Uelimishaji



Mha. David Ngula, Mwenyekiti wa EWURA CCC akimuuliza jambo msimamizi wa Mradi wa umeme wa Rusumo, Mha. Chikwane Mkama wakati Wajumbe wa Baraza walipotembelea Mradi huo hivi karibuni. Picha na Anadorice Komba

Mradi wa umeme Rusumo wapongezwa

Na Anadorice Komba, Kagera

Baraza la Ushauri la Watumaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limepongeza hatua za ujenzi wa Mradi wa kufua umeme wa Rusumo (The Regional Rusumo Falls Hydroelectric Project) unaotekelawa kwa ushirikiano wa nchi tatu za Tanzania, Rwanda na Burundi ambaa mpaka sasa umefikia asilimia 99.

Pongezi hizo zimetolewa hivi karibuni na Mwenyekiti wa Baraza Mhandisi David Ngula wakati ya ziara iliyofanywa na Wajumbe wa Baraza kwenye Mradi huo kwa lemgo la kujiona maendeleo ya Mradi.

Ziara hiyo ilijumuisha Wajumbe na Sekretariati ya Baraza pamoja na Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji ya Mkoani Kagera, huku Mhandisi Ngula akisema kuwa mradi huo ni wa faida, sio tu kwa wakazi wa Rusumo bali kwa watumiaji wa huduma za umeme kote nchini.

"Umeme wa maji una gharama ndogo za uzalishaji ukilinganisha na umeme unaozalishwa kwa vyanzo vingine, hivyo naamini Mradi huo ukikamilika utawanufaisha sio tu

wakazi wa eneo la Mradi huu bali utaonegeza kiasi cha umeme kwa watumiaji wa huduma hiyo kote nchini," alisema Mhandisi Ngula.

Awali akizungumza katika ziara hiyo Mhandisi wa Mradi huo Ndugu Chikwane Mkama kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) alieleza kuwa, ujenzi wa Mradi huo ni wa ushirikiano wa nchi tatu ambazo ni Tanzania, Rwanda na Burundi na utakuwa na uwezo wa kuzalisha jumla Megawati 80 za umeme ambapo kiasi hiki

"Mradi wa Rusumo unaitwa "The Regional Rusumo Falls Hydroelectric Project," ukukamilika utakuwa na uwezo wa kuzalisha jumla Megawati 80 za umeme ambapo kiasi hiki cha umeme tutagawana kwa usawa na nchi washirika ambapo kila nchi itapata wastani wa Megawati 26.66," alisema Mha. Mkama na kuongenza kuwa ujenzi wa mradi huo ulianza rasmi mwaka 2017 na sasa unalekeea kukamilika.

Alisema kwa sasa mradi ume-kamilika kwa kiasi cha asilimia 99, na mashine mbili zimeanza kufanya kazi ambapo Megawati 54 zinazalishwa na kugawanywa kwa usawa katika nchi tatu washirika, huku mashine moja kati ya mashine tatu bado haijawashwa lakini ipo kwenye majoribio na hivi karibuni

itaanza kufanya kazi na kukamilisha megawati 80 za uzalishaji.

Naye Afisa Mazingira na Maendeleo ya Jamii katika Mradi huo Bw. Nassor Mulika kutoka Taasisi inayosimamia ujenzi wa Mradi wa Rusumo, "Nile Equatorial Lakes Subsidiary Action Program" (NELSAP) alisema kuwa Mradi huo haunufaisi tu wananchi kupata huduma ya umeme, bali umetekeleza shughuli mbalimbali za kijamii kuititia mradi wa "Local Area Development Programme" (LADP) kuititia Benki ya Dunia.

"Mradi huu umenafaisha wakazi wa maeneo haya ikiwemo wale walopewa fidia ya ng'ombe na mbuzi. Pia mradi umejenga vyumba vya madarasa, mabweni kwa shule za msingi na sekondari Pamoja na kituo cha afya. Mradi pia umeweza kili-mo cha vitalu (green house), ufugaji wa mbuzi, nyuki, sungura, ng'ombe na kuku kwa wakazi hao," alisema Mulika.

"Sambamba na hayo upo mradi mkubwa wa maji ambaa utaenda kuondoa changamoto ya ukosefu wa majisafi na salama kwa wakazi wanazunguka eneo hili la mradi ambaa umekamilika na utazinduliwa siku za hivi karibuni," alieleza Bwana Mulika.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (RCC) mkoani Kagera, Najim Bwanika alisema ziara hiyo imekuwa ya manufaa kwa Kamati hiyo kwani imeweza kujifunza mambo mengi yanayohusu faida ya mradi huo wa Rusumo kwa wananchi.

"Katika karne hii ya sayansi na teknoljia tunahitaji sana huduma ya umeme wa uhakika. Uchumi imara utajengwa kwa uwepo wa umeme wa uhakika nchini. Nikiri kwamba ziara hii imetu-fungua macho na kutoungezea ufahamu kwa namna Serikali inavyofanya jitihada za kuwa na umeme wa uhakika nchini. Sisi tutaendelea kuwa mabalizi na kutowakilisha vyema watumiaji wa huduma hizi ikiwemo kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kutunza midundombinu na kuthamini miradi kama hii ambayo Serikali inawekeza fedha nyingi," alisema Bwanika.

RCC Singida waipa heko SUWASA

Na Geoffrey Sokesia. Singida

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kuititia Kamati yake ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mko wa Singida (RCC) limeipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA) kwa kuanza ujenzi wa mradi wa mabwawa ya majitaka yanayojengwa katika eneo la Manga, nje kidogo ya Manispaa ya Singida.

Pongezi hizo zimetolewa hivi karibuni na Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mko wa Singida Bi. Bertha Mlingi wakati Kamati hiyo ilipotembelea vyanzo vya uzalilishaji maji na mradi wa majitaka amba kwa sasa upo katika hatua za awali za ujenzi.

Bi. Mlingi alisema ujenzi wa mradi huo utakuwa suluhisho la tatizo la umwagaji majitaka kiholela amba ume-kuwa ukifanywa na watoa huduma binafsi katika mji wa Singida.

"Kwa miaka mingi tumekuwa tukikodi magari ya majitaka kwa gharama kubwa, lakini bila kujua wapi magari hayo yanamwaga maji hayo machafu," alisema Bi. Mlingi.

Alieleza kuwa ujenzi wa mradi huo pamoja na kuwa ni moja ya mkakati wa utunzaji wa mazingira lakini pia utasaidia kupunguza garama kubwa ambazo wananchi wa Manispaa ya Singida wamekuwa wakilipa ili kupta huduma hiyo adimu kwa wafanya-biashara binafsi wa magari ya huduma hiyo.

Kwa upande wake Bi. Evertista Lucas ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mko wa Singida aliiomba SUWASA kuukamilisha mapema mradi huo ili wananchi waanze kunufaika nao.

"Kwa sasa huduma ya majitaka ni changamoto kubwa ndani ya mji wetu wa Singida kwani baadhi ya wananchi wamekuwa wakitapisha mashimo ya vyoo yaliyoja nyakati za mvua jambo ambalo ni hatari kwa afya za watu na mazingira. Hii yote ni kwa kuwa haku-na huduma ya kuaminika ya kuondosha majitaka," alilalamika Bi. Evarista.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja wa SUWASA ndugu Hosea Magimbi alieleza kuwa SUWASA kwa sasa ipo mbioni kukamilisha mradi huo wa majitaka amba pamoja na kutua changamoto ya sehemu ya kumwaga majitaka lakini

pia mabwawa hayo yatakuwa chanzo cha mapato kwa Mamlaka hiyo.

"Kutakuwa na ada ya ukusanyaji majitaka kwani Mamlaka ipo mbioni kununua gari kwa ajili ya huduma hiyo ya ukusanyaji majitaka lakini pia watu binafsi watakaofanya biashara hiyo ya ukusanyaji wa majitaka nao watalipia ada ya kumwaga majitaka katika mabwawa yetu," alisema Bw. Magimbi.

Magimbi aliongeza kuwa majitaka yatakayomwaga kwenye mabwawa hayo yatachakatwa na kutumika tena kwa ajili ya shughuli zingine za kiuchumi kama vile umwagiliaji katika kilimo cha bustani.

Alisema kwenye bwawa kuna maabara ambayo itatumika kufutilia mwenendo wa majitaka ambayo yat-amwagwa na kuchakatwa kwa ajili ya matumizi mengine.

Mkurugenzi huyo alibainisha pia kuwa kwa siku za usoni SUWASA ina mpango wa kujenga mtandao wa majitaka ndani ya Manispaa ya Singida ambapo wateja wataunganishiwa huduma hiyo badala ya kila nyumba kuwa na shimo la majitaka.

Ndugu Hosea Magimbi, Mkurungezi wa Huduma kwa Wateja SUWASA, akiwaeleza jambo Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mko wa Singida hivi karibuni walipotembelea Mradi wa ujenzi wa Mabwawa ya kuhifadhi Majitaka unaotekelwa katika eneo la Manga Manispaa ya Singida.

Picha na Evarista Lucas



Unaweza kufidiwa ukiathirika na gesi



Na Sakina Yusuf, Tabora

Gesi ni moja kati ya nishati zinazotumiwa kwa wingi majumbani kwa kupikia kwani mbali na kutunza mazingira pia inaokoa muda wa

mtumiaji kukaa jikoni.

Wengi wa watumiaji hutumia gesi za petroli (Liquidified Petroleum Gas (LPG) kwani ndio hupatikana kwa urahisi na katika maeneo mengi nichini. Licha ya manufaa yake kwa mtumiaji, tahadhari zin-

Mitungi ya ujazo mbalimbali ikiwa inajazwa gesi katika moja ya vituo vya kujazia gesi. Picha kwa hisani ya Tanzania sasa Blogspot



www.tanesco.co.tz

PATA TAARIFA NA HUDUMA MBALIMBALI ZA TANESCO KUPITIA MITANDAO YETU YA KIJAMII

 [tanesco_official_page](#) [Tu follow](#)
 [@tanescoyetutz](#) [Tu follow](#)
 [www.tanesco.co.tz](#) [Peruzi](#)
 [0758346869](#) [Chat](#)

Tafadhalili tupatia taarifa kamili kwa huduma bora.

[#Tupokazini](#)






UJUMBE KWAKO MPENDWA MTEJA



Kuwa na utaratibu wa kusoma MITA ili kujua matumizi yako ya maji na kupata ankaru sahihi

Zoezi la usomaji mita yako linaendelea TUWASA inaoomba ushirikiano katika kipindi hiki cha usomaji.

www.tuwasa.go.tz [0800780063](#)

atakiwa zichukuliwe katika uhifadhi na matumizi yake ili kuepusha madhara kwa watumiaji.

Baadhi ya madhara yanayoweza kusababishwa na nishati ya gesi pindi inapotumiwa na kuhifadhiwa bila tahadhari ni pamoja na kuharibu mali, mazingira na hata kupelekeaa kupoteza uhai wa watumiaji pale ikitokea gesi hiyo imelipuka.

Makala hii inalenga kuwakumbusha watumiaji wa gesi ya kupikia majumbani kutambua haki zao za msingi ikiwemo haki ya kudai fidia pindi mtumiaji akipata hasara au kudhurika na bidhaa za gesi (LPG).

Kutokana na unyeti wa huduma hiyo, Sheria ya Petroli chini ya Kanuni za Uendeshaji Huduma za Gesi za Petroli za mwaka 2020, Tangazo la Serikali namba 825 la tarehe 2 Oktoba 2020 iliweka kipengele ki-

nachohusiana na kulinda maisha ya watu na mali zao.

Kwa mujibu wa Kanuni hii, wasambazaji wa gesi hizi za petroli wanatakiwa kuchukua tahadhari ili kutohatarisha usalama wa afya za watumiaji na mali zao kama inavyoonekana katika Kanuni ya 22(1) ikielekeza kwamba wasambazaji wakubwa na wadogo wachukue tahadhari wakati wa kuhifadhi, kuihudumia, kuitumia, kubeba na kutoiharibu mitungi ya gesi ili kuepuka kuhatarisha usalama na afya za watu na mali zao sambamba na kuepuka uharibifu wa mazingira.

Kanuni hizo zimeweka wazi kwamba endapo kutatokea madhara yoyote basi wasambazaji watawajibika kulipa fidia kwa waathirika wa madhara au hasara itakayosababishwa na gesi.

Kanuni ya 23 (1) (2) (3) zikisomwa kwa pamoja zinatoa utaratibu wa kudai fidia kwa mtu yeyote aliyepata hasara kutokana na madhara ya bidhaa ya gesi kuwa anaweza kuwasilisha lalamiko lake kwa msambazaji wake ili kupata muafaka na endapo lalamiko alilowasilisha kwa mujibu wa Kanuni 23(2) litashindikana basi lalamiko litapelekwa EWURA kwa ajili ya kupata maamuzi zaidi.

Hata hivyo, ili kupata fidia hiyo ni lazima mwathirika kufuta utaratibu sahihi wa kuwasilisha malalamiko ikiwemo kuwasilisha kwa maandishi lalamiko lake na kuwa na risiti ya manunuzi ili kuweza kupata haki yake. Ni muhimu watumiaji wa LPG kuwa waangalifu na kuzingatia matumizi sahihi na salama ya nishati hiyo.



MAMLUKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA TABORA (TUWASA)



**Ndugu mteja ukiokota vifaa vya miundombinu ya maji
Kama vile Dira ya maji, Gate valve, Koki, bomba
Au mpira n.k. Tafadhali wasilisha vifaa
Hivyo ofisi za TUWASA**

ONYO

“Hairuhusiwi kuvihifadhi nyumbani”



Koki



Dira ya Maji



Gate valve



Mpira wa maji

**PIGA BURE
0800780063**

tuwasa_tabora

tuwasatabora



Zingatieni matumizi sahihi ya umeme, maji kupunguza gharama

Na Waandishi wetu, Mwanza na Dodoma

Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mahina iliyopo jijini Mwanza wameombwa kuwasaidia wazazi wao kupunguza gharama kubwa za matumizi ya huduma za umeme na maji kwa kujelimisha kuhusu matumizi bora ya huduma hizo.

Hayo yamesemwa na Bi. Josephine Ntaumenya, Afisa Msaidizi Huduma kwa wateja na Utawala kutoka ofisi ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoani Mwanza wakati Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji ya Mkoa wa Mwanza ilipozuru shule hiyo kwa lengo la kutoa elimu kwa walimu na wanafunzi juu ya umuhimu wa matumizi sahihi ya huduma za maji na nishati.

Katika programu hiyo Bi. Ntaumenya aliwashangaza walimu na wanafunzi kwa kutoa mifano halisi ya jinsi matumizi sahihi ya maji na nishati vinavyoweza kubadilisha gharama za huduma ya maji na

nishati katika familia na jamii kwa ujumla.

Alisema kuwa wanafunzi na walimu ni kada muhimu ya kuelimisha jamii yao kuhusu umuhimu wa rasilimali hizi ili ziwe na uelewa wa kuzingatia matumizi sahihi ya huduma huku akihimiza watumiaji kudai huduma zilizo bora.

"Yawezekana kwa umri wenu sasa hivi hamjui maumivu ya kulipia gharama za huduma hizi lakini miaka ijayo mtakuwa wakubwa nanyi mtaanza kuwajibika katika ulipaji wa bili, hivyo niwaase kutumia huduma hizo kwa umakini kwani kufanya hivyo mtakuwa mnawasiadnia wazazi wenu kuokoa pesa ili zitumike kwa ajili ya majukumu mengine ya kifamilia," alisema Bi. Ntaumenya na kuongeza kuwa, wakati wa usiku watoto wanapokuwa sebuleni wakiangalia TV ni vyema kuzima taa ambazo zipo kwenye vyumba ambavyo havitumiki kwa wakati huo kwani kwa kufanya hivyo utakuwa unaokoa umeme ambaeo ungetumika bila faida ye yeyote ndani ya vyumba."

Akitoa neno lake la shukrani Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo Bi.

Bi. Josephine Ntaumenya, Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala, EWURA CCC Mwanza, akitoa elimu juu ya matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Mwananchi wakati wa programu ya uelimishaji mashulen. Picha na Mpigapicha Wetu

Editha Alfred alionesha hamu ya kutaka elimu hiyo kuwa endelevu akipendeleza isambazwe kwenye jamii yao na hata kufika mitaani ambako wao wanaishi ili kuweza kuifikia jamii kwa mapana zaidi.

"Elimu hii ni muhimu sana kwa jamii yetu na tungependa kushirikiana na Kamati yenu ili kuieneza kwa wazazi na watu wengine katika mazingira yetu ili kila mtu aweze kufaidika," alisema mwalimu Editha.

Kwa upande wao, wanafunzi wa shule hiyo walionekana kufurahia elimu waliyoipata na kuwa na shauku kubwa ya kujifunza zaidi.

Akiongea kwa niaba ya wanafunzi wenzake, Lucia Alfred aliahidi kuvashirikisha wazazi/walezi na jamii inayowazunguka kuhusu matumizi sahihi ya huduma.

"Tutawashirikisha wazazi wetu na majirani kuhusu mambo tulio-jifunza na tutahakikisha kuwa tunawakumbusha wanafunzi wenzetu umuhimu wa matumizi sahihi ya nishati na maji," alisema Lucia.

Katika hatua nyininge mkoani Dodoma, Ndugu Amani Mbogo ambaye ni Afisa Msaidizi Huduma kwa

Twen'zetu na nishati safi ya kupikia

Na Chipegwa Samwel, Morogoro

wateja na Utawala wa EWURA CCC mkoani Dodoma aliwfunda Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata za Dodoma mijini kuhusu matumizi bora ya huduma ya maji yanavyoweza kuwapa unafuu kwenye suala la gharama.

Aliwaeleza Maafisa hao kuwa watumiaji wengi hupoteza maji mengi wakati wa kuoga au kuosha vyombo pindi wanapoyaacha yakinirika kwa muda mrefu hali ambayo huongeza upotevu wa maji na kuongeza gharama kwa mtumiaji pasipo kufahamu.

"Badala ya kufunga bomba la maji na kuosha chombo kimoja, ni vyema kuosha vyombo vingi kwa wakati mmoja kwa kutumia beseni ambalo unakuwa umekinga maji ya kutosha, njia hii husaidia kupunguza upotevu wa maji na hivyo kupunguza gharama ambazo si za lazima," Eileeleza ndugu Mbogo.

Akiongea kwa niaba ya Maafisa hao, Afisa Maendeleo ya Jamii wa Dodoma Mjini, Bi. Charity Sichona aliishukuru EWURA CCC Dodoma kwa kuwapatia elimu yenye manufaa maafisa hao na kusema elimu hiyo itasaidia pia kumpunguza malalamiko ambayo muda mwininge yalikuwa yanatokana na wananchi wenyewe kutumia huduma hizo vibaya.

"Tunawashukuru sana kwa kuja kutuelimisha kuhusu matumizi bora ya huduma hizi. Natumai maafisa wangu watakuwa ni mabalozi wazuri kwa wananchi wao sababu sisi tunakutana na makundi mengi kwenye kazi zetu hivyo ni rahisi sana kufikisha elimu hii kwa uharaka zaidi. Tutaendelea kushirikiana zaidi ili tuwe msaada kwa jamii ya Watanzania wenzetu kwa kufikisha elimu hii kwao," alisema Bi. Charity.

Kamati za watumiaji mkoa wa Mwanza na Dodoma zitaendelea kutoa elimu kwa watumiaji juu ya matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji kwenye mitaa na maeneo mengine ili kuhakikisha wananchi katika maeneo hayo wanufaika na elimu hiyo.

Gesi itumikayo majumbani ni mojawapo ya nishati safi ya kupikia ambayo baadhi ya watumiaji wamekuwa wakiitumia siku hadi siku kutokana na uharaka na uhakika wake.

Gesi nyingi itumikayo majumbani kwa sasa ni zao litokanalo na kusafishwa kwa mafuta ghafi (crude oil), ambayo ipo kwenye mfumo wa kimiminika na huifadhiwa kwenye mitungi. Gesi hii inaundwa na kemikali za aina mbili ambazo ni 'butane' na 'propane'. Kwa kiasi kidogo matumizi ya gesi asilia yameanza kutumika hasa katika Mkoa wa Mtwara.

Katika harakati za utunzaji mazingira, mataifa mbalimbali duniani yamekuwa yakisisitiza matumizi ya gesi ya kupikia ili kuondokana na uharibifu na uchafuzi wa mazingira.

Serikali ya Tanzania imeanzisha kampeni ya uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi ikiwemo LPG na kuwa na "Dira ya Taifa ya Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia 2033." Dira hii inatamka kuwa kila Mtanzania atumie nishati safi ya kupikia ili kuboresha afya na kulinda mazingira. Jitihada zote hizi ni kuonesha umuhimu wa matumizi ya nishati hii kwa shughuli za kupikia.

Makala hii imelenga kubainisha sifa nzuri na changamoto katika kutumia nishati ya gesi ya kupikia (LPG).

Nishati safi ya kupikia ya gesi ina sifa zifuatazo:

- Haina rangi wala harufu kwenye mfumo wake wa asili. Harufu huwekwa wakati inajazwa kwenye mitungi ili kumpa urahisi mtumiaji kugundua kama inavuja.

- Ni nzito kuliko hewa na ipo kwenye mfumo wa maji, hivyo ikivuja hushuka chini.

- Inatakiwa ihifadhiwe kwenye chumba chenye kuruhusu hewa kuingia na kutoka nje kwa ajili ya kuepusha athari za moto.

■ Ikichanganyika na hewa inakosa nguvu.

■ Inawaka inapokutana na chanzo cha moto.

■ Haiharibiki (haina expiry date), hivyo inaweza kukaa kwa muda mrefu.

■ Inaweza kutumika kupikia, kukatia vyuma, na hata kuendesha injini na jenereta kwa sababu inaungua taratibu kuliko mafuta.

■ Haitoi masizi kwenye vyombo vya kupikia.

■ Ni rafiki kwa mazingira kwa kuwa inapunguza matumizi ya mkaa au kuni.

■ Ni rafiki kwa afya tofauti na moshi wa kuni.

■ Ni rahisi kuisafirisha bila kuleta madhara.

Changamoto katika matumizi ya nishati hii:

- Kupanda na kushuka kwa bei ya gesi kunakotokana na mabadiliko ya bei kwenye soko la dunia.

- Inaweza kusababisha ajali ya moto endapo ikivuja na ikakutana na mazingira ya kuchocheara moto.

- Ikivutwa yaweza kusababisha mtu kufa kwa kukosa hewa safi, "suffocation" na kuharibuu mfumo wa hewa kwenye mwili.

EWURA CCC inao mchangano wa moja kwa moja katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya matumizi ya nishati safi ya kupikia. Katika kuthibitisha hili, kupitia programu zake za uelimishaji, Baraza litaendelea kuhamasisha umma juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi ya nishati hiyo.

Dira ya taifa ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ilizinduliiwa rasmi hapa nchini mwezi Juni 2023 na Waziri wa Nishati wa kipindi hicho Mhe. January Makamba, ambapo aliainisha masuala mbalimbali ikiwemo hatua ambazo Serikali itachukua ili kuwezesha asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2033.

Makala

Washauriwa kulalamikia huduma mbovu

Na Mwandishi wetu, Geita

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoani Geita lime-waomba wananchi mkoani humo kuacha kunung'unika kutohana na huduma mbovu wanazozipata kutoka kwa watoa huduma za nishati na maji na badala yake wapeleke malalamiko yao kwa watoa huduma husika na nakala kwa ofisi ya EWURA CCC Mkoa wa Geita kwa ajili ya ufuatilaji na utatuzi.

Hayo yamesemwa na Mwenyekiti

wa Kamati ya Baraza ya Watumiaji Mkoa wa Geita ndugu Dotto Paul wakati akitoa elimu kwa wananchi walitembelea banda la EWURA CCC kwenye maonesho ya sita ya kitaifa ya teknolojia ya madini yaliyofanyika katika viwanja vya EPZ Bombambilii katika halimashauri ya mji wa Geita mwishoni mwa Septemba 2023.

Ndugu Dotto alisema baadhi ya wateja wanaotumia huduma za umeme, bidhaa za petrol, gesi na maji wamekuwa wakipata changamoto ya huduma mbovu kama vile kupata umeme wenye nguvu kupitiliza, kupata umeme mdogo, kuchelewa

kuunganishiwa huduma lakini hata hivyo wamekuwa hawalalamikii changamoto hizo wanazopitia bada la yake wamekuwa wakinung'unika tu.

"Niwasihii kuwa pindi mnapokuwa na malalamiko, msiishie kunung'unika tu bali chukueni hatua za kuandika malalamiko yenu na kuyawasilisha kwa watoa huduma, na kuleta nakala ya lalamiko kwenye ofisi za EWURA CCC kwa ajili ya ufuatilaji na hatimaye utatuzi wa malalmiko hayo," alieleza ndugu Dotto.

Naye ndugu Juma Hamisi, mkazi wa Kata ya Buhalahala ambaye ni miiongoni mwa wananchi walitembelea banda la EWURA CCC wakati wa maonesho hayo na kupata elimu, alisema kuwa wananchi wengi ambao ni watumiaji wa huduma za nishati na maji hawana uelewa wa kutosha wa namna gani ya kulalamikia huduma mbovu zinazotolewa na watoa huduma wa umeme, maji, gesi hata mafuta.

"Kwa kweli sisi tunapopata shida ya huduma za nishati na maji baadhi tunashindwa kulalamika kwa kuwa hatuna elimu sahihi ya kulalamikia huduma mbovu. Kwa elimu hii tulioipata kutoka EWURA CCC imetuungezea uelewa wa hatua za kuchukua pindi tunapopata changamoto za huduma hizi," alieleza ndugu Hamisi.

Alisema anaishukuru EWURA CCC kwa kufika katika maonesho hayo na kutoa elimu huku akiiomba kuendelea kutoa elimu zaidi kwa watumiaji wa huduma za nishati na maji ili kuongeza ufahamu miiongoni mwa watumiaji kuhusu huduma hizo.

Kwa mujibu wa sheria ya kuanzishwa kwake, moja ya majukumu makuu ya EWURA CCC ni kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji kwa kutoa elimu kwa watumiaji kuhusu huduma hizo pamoja na kuwawakilisha katika vyombo vya maamuzi ikiwemo Wizara pamoja na EWURA pindi kunapokuwa na masuala yanayogusa maslahi mapana ya watumiaji wa huduma hizo.



Ndugu Jacob Steven, Mwenyekiti wa Mtaa wa Mwatulole Geita (wa kwanza kushoto) akielezea jinsi wananchi wa Mtaa wake walivyofaika na elimu walivoipata kutoka EWURA CCC kuhusu matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji alipotembelea banda la Baraza wakati wa maonesho ya Dhahabu yaliyofanyika Oktoba 2023 katika viwanja vya Bombambilii, mijini Geita. Picha na Mpigapicha Wetu

Toeni elimu matumizi ya gesi - EWURA CCC

Na Mwandishi wetu, Tanga

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoani Tanga limeitaka kampuni ya usambazaji wa gesi ya kupikia ya Orxy kutoa elimu ya matumizi ya gesi kwa wateja wake ili kuokoa pesa na kupunguza majanga ya moto.

Wito huo umetolewa hivi karibuni na Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala wa EWURA CCC Mkoa wa Tanga Bi. Nuru Zuberi wakati aliposhiriki semina iliyofanyika jijini Tanga ambayo iliandaliwa na Kampuni ya Usambaziji gesi za kupikia ya "Oryx Gas Tanzania" lengo likiwa ni kutoa elimu ya matumizi bora na sahihi ya gesi kwa wateja wake amba ni wauzaji wadogowadogo.

Elimu iliyotolewa ni pamoja na upimaji sahihi wa mitungi ya gesi, jinsi ya kuhifadhi mitungi hiyo gesi na njia sahihi za kufuata unapogundua kuna uvujaji wa gesi.

Bi. Nuru alisema kuwa pamoja na kuwapa elimu wauzaji wa gesi pia aliwaomba Orxy na wauzaji wadogo kuendelea kutoa elimu sahihi kuhusu matumizi na uhifadhi wa gesi kwa watumiaji kwani kwa kufanya hivyo watakuwa wanapunguza malalamiko

juu ya changamoto zinazotokana na bidhaa hiyo.

"Ninawapongeza Orxy kwa kuandaa semina hii kwa kuwa ikizingatiwa na washiriki itapunguza kasi ya malalamiko kwa wateja wao. Niwaombe wauzaji wadogo wa gesi huko katika mitaa yetu kuwapatia wananchi elimu juu ya matumizi sahihi na salama ya gesi. Hii pia itachochaea wananchi kutumia gesi zaidi na kuondokana kabisa na matumizi ya kuni na mkaa ambayo ni hatari kwa mazingira," alisema Nuru.

Pamoja na wito huo, Bi. Nuru alitumia fursa hiyo kutoa elimu kwa washiriki wa semina hiyo juu ya matumizi sahihi ya gesi ya majumbani ikiwemo mambo yanayoweza kusababisha matukio ya moto na hasara majumbani na namna ya kuokoa pesa kupitia matumizi sahihi ya gesi.

"Elimu hii ya matumizi sahihi ya gesi itawasaidia sio tu kuokoa pesa zenu bali hata usalama wenu majumbani. Ni muhimu kupima ujazo wa mitungi mnaponauzia wateja wenu au ninyi mnaponunua ili kuona kuwa pesa mnazolipa zinaendana na bidhaa husika. Pia ni muhimu kuwa na vifaa vya kuzima moto majumbani kwa ajili ya kukabili mlipuko wa moto unaoweza kusababishwa na mvujo wa gesi," aliongeza Bi. Nuru

Kwa upande wake Afisa Masoko wa Kampuni ya ORYX Mkoa wa Tanga Bw. Andrew Noel alipokea ushauri toka EWURA CCC na kuahidi kuendelea kutoa elimu kwa wauzaji na watumiaji kila itakapohitajika.

"Tumepokea ushauri na maoni ya Baraza na pia tunashukuru kwa ushiriki wenu kwenye semina hii. Tunaahidi kuendelea kutoa elimu hii mara kwa mara kwa wauzaji wetu ili waweze kuwahudumia ipasavyo walaaji wa mwisho," alisema Noel.

Kwa upande wa mwakilishi wa wauzaji wadogo wa gesi za majumbani kutokea Donge ndugu Salum Zahoro amelipongeza Baraza kwa kuwapa elimu kupitia semina hiyo ikiwemo kuzima vifaa vya umeme pindi gesi inapovuja.

"Binafsi nimeongeza elimu kwani sikuwahi kujua kuwa kuwasha swichi ya umeme ni hatari pindi gesi inapovuja. Nawashukuru waandaji wa semina hii lakini pia naishukuru EWURA CCC kwa elimu nzuri mliyutupa leo," alisema Bw. Zahoro.

Bw. Zahoro alihitimisha kwa kuuomba uongozi wa Kampuni ya ORYX kuendelea na utamaduni huo wa kutoa elimu kwa mawakala wake ili kuwajengea uwezo wa kuwahudumia wateja wao kwa usalama na ubora zaidi kuhusu huduma zao.



Bi. Nuru Zuberi Afisa, Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala EWURA CCC Mkoa wa Tanga, akigawa vipeperushi wakati wa semina kwa wauzaji wadogo wa gesi za kampuni ya Oryx mapema Septemba 2023 mjini Tanga ambapo Ofisi ya EWURA CCC ilishiriki na kutoa elimu juu ya matumizi sahihi ya gesi. Picha na Mpigapicha Wetu

Majalamiko

HabariPicha



Mha. David Ngula, Mwenyekiti wa Baraza, akitoa neno la shukrani wakati wa kuhitimisha kikao-kazi kati ya Wajumbe wa Baraza na watumishi wake na Maafisa kutoka Wizara ya Nishati kilichofanyika Bagamoyo mkoani Pwani. Picha zote na Mpigapicha Wetu



Bi. Stella Lupimo, Kaimu Katibu Mtendaji wa EWURA CCC, akitoa maneno ya utangulizi wakati wa kikao-kazi kati ya Wajumbe wa Baraza na Kamati ya "Think Tank" kutoka Wizara ya Nishati.



Mha. David Ngula (aliyeketi katikati), Mwenyekiti wa EWURA CCC akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Baraza baada ya kikao cha mwaka 2023. Kulia ni Bi. Stella Lupimo, Kaimu Katibu Mtendaji wa EWURA CCC na Erasto Kishe, Mhasibu wa Baraza.



Mha. Nyirabu Musira, Meneja Kanda ya Mashariki EWURA
aliyemwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, akiongea wakati wa kikao-
kazi kilichokutanisha Wajumbe wa Baraza, Wafanyakazi na Maafisa kutoka
Wizara ya Nishati kilichofanyika Agosti 2023 mjini Bagamoyo.



Picha ya pamoja ya Wajumbe wa "Think Tank" ya Wizara ya Nishati na wawakilishi kutoka
EWURA CCC walipokutana hivi karibuni kujadili masuala mtambuka ya Baraza. Walioketi,
katikati ni Mha. Pius Mabuba, Mjumbe EWURA CCC, Kulia ni Bw. Wilson Nyamanga, Mwenyekiti
Kamati ya Think Tank na kushoto ni Bw. Ephata Lolubo, Mchumi Mkuu kutoka EWURA.



Ndugu Mohamed Kasim, mwendesha mitambo (pump operator) wa Mamlaka ya
Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA) akitoa maelezo kwa Wajumbe
wa RCC Singida walipotembelea chanzo cha maji kilichopo Mwankoko.

Baraza lafutilia utatuzi wa kero Mgaza



Wakazi wa mtaa wa Mgaza wakiendelea na zoezi la kuchimba mtaro kwa ajili ya uboreshaji miundombinu ya maji katika mtaa wao. Picha na Jasper Mallya

Na Chipegwa Samwel, Morogoro

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA CCC) Mkoa wa Morogoro limeshiriki katika kufutilia utatuzi wa kero ya ukosefu wa huduma ya maji ulioathiri kaya 43 za mtaa wa Mgaza.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya mwakilishi wa waathirika hao ndugu Rajabu Kitundu maarufu kwa jina la "Mjeshi" kufika ofisi za EWURA CCC Morogoro mwezi Septemba 2023 kwa lengo la kuwasilisha lalamiko lao juu ya changamoto ya ukosefu wa huduma ya maji katika eneo la hilo.

"Tuna muda mrefu sana hatupati huduma ya maji, tumefutilia mara kadhaa katika ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) lakini hadi leo bado tunaenedelea kupata changamoto hii ya kutopata huduma ya maji," alisema ndugu Kitundu.

Katika kufutilia utatuzi wa lalamiko hilo, Ofisi ya EWURA CCC Morogoro ilifanya mawasiliano na Afisa Huduma kwa Wateja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) Bi. Joyce Nyangoya ambaye alikiri kuwepo kwa changamoto hiyo huku akisema ilijitokeza baada ya kubainika kuwa mizizi ya mti ilikuwa imekandamiza mpira wa maji uliosababisha kuko-sekana kwa huduma hiyo.

Bi. Nyangoya alieleza pia kuwa kulikuwepo na mivujo mikubwa ambayo ilibainika kwenye mashamba yanayomilikiwa na Chuo cha Kilimo cha Sokoine (SUA) ambako njia ya maji imepita na kupelekea upunguwa maji kwa wateja hao.

"Fundii wetu amethibitisha kuwa kwenye eneo hilo kulikuwa na changamoto ya mzizi wa mti kukandamiza bomba linalopeleka maji kwa wateja na vile vile kulikuwa na mivujo kadhaa kwenye eneo la mashamba ya chuo cha SUA ambako laini ya maji kwenda kwa wateja hao imepitaa na hivyo kupelekea kasi ya maji kupungua kufika kwa wateja wetu wa eneo hilo," alieleza Bi. Nyangoya.

"Changamoto hizo tume-shazidhibiti na tumpanga kuwa-

tembelea wateja hao siku ya zamu zao ili kujiridhisha na hali halisi ya upatikanaji wa maji," aliongeza.

Katika jitihada za kutatua changamoto hiyo Meneja wa Kanda wa eneo hilo wa MORUWASA Bw. Michael Kingazi pamoja na Afisa kutoka ofisi ya EWURA CCC Morogoro waliamua kutembelea eneo hilo kwa lengo la kufuatilia na kujionea changamoto hiyo ya ukosefu wa maji.

Wakati wa ziara hiyo Kingazi aliwaarifu wakazi wa eneo hilo kuwa ziara hiyo ilikuwa na lengo la kufuatilia changamoto ya ukosefu wa huduma wanayoipata wateja na hatimaye kuja na suluhisho.

"Tumejionea wazi kuwa kuna baadhi ya maeneo maji yanafika na sehemu zingine bado hayafiki kwa wingi, hivyo tutaenda kukaa na wataalamu wenzetu ili kuishauri Menejimenti juu ya kuboresha upatikanaji wa huduma hii muhimu katika Maisha ya kila siku. Tunakusidia kubaini maeneo yote yanayotakiwa kufanyiwa maboresho, na kutathmini ni mabomba yenye

“

Lengo letu ni kutaka

maji yapatikane, hivyo tutafanya uboreshaji wa miundombinu, kuweka ratiba ya upatikanaji wa huduma na kuachilia maji katika maeneo haya. Tunawasihi muwe wavumilivu kwa suala hili linategemea bajeti kwa ajili ya gharama za mabomba na shughuli ya uchimbaji mitaro ya kulaza bomba, mambo ambayo yanaweza kuchukua muda kidogo

kipenyo gani yatandikwe katika eneo hili," alifafanua Bwana Kingazi.

Katika kuhitimisha maelezo yake, Bwana Kingazi aliwaahidi wananchi wa eneo hilo kwa kusema kuwa, "lengo letu ni kutaka maji yapatikane, hivyo tutafanya uboreshaji wa miundombinu, kuweka ratiba ya upatikanaji wa huduma na kuachilia maji katika maeneo haya. Tunawasihi muwe wavumilivu kwa suala hili linategemea bajeti kwa ajili ya gharama za mabomba na shughuli ya uchimbaji mitaro ya kulaza bomba, mambo ambayo yanaweza kuchukua muda kidogo."

Katika kuonesha kuchosha na kero hiyo wakazi wa eneo hilo walimuahidi Meneja huyo wa MORUWASA kuwa wao wapo tayari kujitolea kuchimba mitaro kama mabomba yatakuwepo ili waweze kupata huduma hiyo kwa haraka.


EWURA CCC kuititia Kamati yake mkoani Morogoro itaendelea kufuatilia kwa karibu utatuzi wa changamoto hiyo ili kuhakikisha huduma inarejea katika eneo hilo.

Je wajua?

MORUWASA

Inadhamana ya kutoa huduma ya kusambaza Majisafi na Usafi wa Mazingira katika maeneo ya

- **Manispaa ya Morogoro**
- **Mji wa Kilosa**
- **Mji wa Mikumi**
- **Dumila**
- **Dakawa**
- **Mzumbe**
- **Mkambarani**
- **Mkono wa Mara na Pangawe**



www.moruwasa.go.tz



@moruwasa

@moruwasa2



0736 737 736



0800751011 (BURE)

Uandaaji Mkataba wa Huduma kwa Wateja uwe shirikishi

Na Dennis Ndanu, Mara

Bazaza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kuititia Kamati yake ya Watumiaji ya Mkoa wa Mara wameishaari Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) kuwashirikisha wateja wake katika mchakato mzima wa kutengeneza Mkataba wa Huduma kwa Mteja.

Ushauri huo umetolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Mara (RCC) ndugu Robinson Wangaso wakati Kamati yake iliposhiriki kikao kilichoitishwa na MUWASA kwa ajili ya kutoa maoni juu ya mchakato wa kuandaa Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa Mamlaka hiyo.

Wangaso amesema ni vyema MUWASA kushirikisha wateja wake wakati wa uandaaji wa mkataba huo ili wateja wajue na kuyaelewa yaliyomo katika Mkataba huo huku akiomba MUWASA kuipa muda wa kutosha Kamati yake ili kuisoma rasimu ya Mkataba huo ili iwe na maoni yenye tija katika kuimarisha ubora wa huduma zinazotolewa na

Mamlaka hiyo.

"Wananchi walio katika maeneo yanayohudumiwa na MUWASA ni kundi muhimu ambalo linaguswa na mkataba huu na wale walio wateja ya MUWASA tayari unawahu moja kwa moja, hivyo ni muhimu kuwashirikisha katika maandalizi ya mkataba huu."

"Wateja wenu wanayo maoni mengi ambayo kama watasikilizwa watachangia kupatikana kwa Mkataba wenye tija na masilahi kwa pande zote mbili. Ni muhimu pia kuwe na muda wa kutosha kukusanya maoni ya wadau kwa ajili ya kupata Mkataba bora," alifafanua Wangaso.

MUWASA iliitisha kikao hicho kwa lengo la kuwasilisha rasimu ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja ambapo katika kikao hicho Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, viongozi wa dini na asasi za kiraia kutoka katika Manispaa ya Musoma mkoani Mara walialikwa na kushiriki.

Ndugu William Patrick Gumbo, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Musoma ambaye alikuwa mionganoni mwa viongozi walioshiriki kikao hicho alisema MUWASA ina wajibu wa kuwashirikisha watumiaji kwa kutoa elimu kwa wateja wake kuhusu mkataba huo

wanaouandaa.

Alisema "nashauri MUWASA itengeneze vipeperushi vya rasimu ya mkataba huo unaopendekezwa na vigawiwe kwa viongozi wa mitaa yote ndani ya Manispaa yetu ili nao wawashirikishe wananchi katika mitaa yao kisha maoni yatakayopatikana yafanyiwe kazi kwa ukamili."


Kwa upande wake Kaimu Mkrugenzi wa MUWASA ndugu Geervas Nikas Mugisha aliwashukuru wajumbe wa kikao hicho kwa ushauri wao ambaa waliutoa na kuahidi kuwa Mamlaka hiyo itazingatia na kutekeleza mapendelekezo hayo hatimaye kuweza kupata maoni mengi zaidi yatakayosaidia kuboresha Mkataba wa Huduma kwa Wateja kabla ya kuanza kutumika.

Mbali na kuwasilisha rasimu hiyo, Ndugu Mugisha pia aliwadokeza wajumbe wa kikao hicho nia ya MUWASA ya kuanza mchakato wa kurekebisha bei za maji kwa watumiaji wa makundi yote mara baada mkataba wa huduma kwa wateja kukamilika.

"Ndugu zangu naomba pia kuwaeleza kwa kifupi kuwa baada ya kukamilisha zoezi la kupata Mkataba wa Huduma kwa Wateja, tunatarajia kuanzisha mchakato wa kurekebisha bei za huduma ya maji kwa makundi mbalimbali ya watumiaji ikiwa ni hatua mahususi ya kuendelea kutoa huduma bora na endelevu," alisema Mugisha.



Mhe. William Patrick Gumbo, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Musoma akizungumza wakati wa kikao-kazi cha mchakato wa kutoa maoni kuhusu maboresho ya Rasimu ya Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA). Katika picha, kulia ni Mhe. Magiri Benedict Maregesi, Mwenyekiti wa CCM wilaya ya Musoma na kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa MUWASA Mha. Nikas Gervase Mgisha. Picha na Mpigapicha Wetu



Afisa mazingira wa kata ya Bomambuzi Bwana Yahaya Mndeme akionyesha bomba linalovuja maji eneo la Pasua mtaa wa Sokoni, Moshi Picha na Mpigapicha Wetu

Ushauri

MUWSA yashauriwa kuhusu upotevu wa Maji

Na Zamda Mabada, Kilimanjaro

Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoani Kilimanjaro, ndugu William Luanda ameishauri Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi (MUWSA) kufatuta namna bora ya kuzuia tatizo la upotevu wa maji unaosababishwa na kupasuka kwa mabomba ya maji na hivyo kusababisha ukosefu wa huduma hiyo kwenye baadhi ya maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka hiyo.

Ushauri huo umetolewa hivi karibuni kufuatia malalamiko kutoka kwa wakazi wa Manispaa ya Moshi yaliyotolewa kwa nyakati tofauti wakati wa programu za uelimishaji zinazofanywa na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kwa makundi mbalimbali kwenye Manispaa hiyo.

Akiongea kwa niaba ya watumiaji, Mwenyekiti huyo alishauri Mamlaka hiyo kuhakikisha kuwa inadhhibitit upotevu wa maji ili huduma hiyo iwfafiki watumiaji wengi huku ikizua upotevu wa mapato unaosababishwa na upotevu wa maji.

"Tunaishauri MUWSA kudhibiti upotevu wa maji ili kuwafanya wateja wapate huduma na kuepusha MUWSA kupata hasara. Pia tunaomba muendelee kuwapatia watumiaji elimu kuhusu umuhimu wa kulinda miundombinu ya maji ikiwemo utayari wa kutoa taarifa pindi wanapoona maji yanavuja," alisema Luanda.

Akielezea kuhusu changamoto hiyo Mhandisi Innocent Lugodisha ambaye ni Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usimamizi wa Mazingira MUWSA alikiri kuwa tatizo la upotevu wa maji ndani ya Mamlaka hiyo lipo ambapo kwa miaka ya hivi karibuni limefikia asilimia 24 ikiwa ni zaidi ya kiwango kinachokubalika cha asilimia 20.

"Wastani huu wa asilimia 24 umeongezeka kutoka 20.1 kwa kipindi cha nyuma, hii ni kutokaza na changamoto ya uchakavu wa miundombinu baada ya Mamlaka yetu kuongezewa eneo la kuhudumia la Moshi vijijini kwa kata 12 pamoja na vijiji viwili kutoka wilaya ya Hai vilivyokuwa vinahudumiwa na Jumuiya mbalimbali za maji zilizoko chini ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, RUWASA," alieleza Mhandisi Lugodisha.

Alisema kuwa, baada ya MUW-

SA kukabidhiwa maeneo mapya nje ya Manispaa ndipo walipokutana na changamoto za miundombinu mibovu ikiwemo mabomba, pia wateja zaidi ya 3,000 hawakuwa wamefungiwa dira za maji ambayo ilisababisha tatizo la upotevu wa maji hadi kufikia asilimia 24.

"Mamlaka ilibainisha changamoto hizo nasi tukaja na mkakati wa kuelimisha watumiaji kuhusu umuhimu wa kutunza miundombinu ya maji pamoja na kuwafungia mita za maji kwa kushirikiana na viongozi mbalimbali wa maeneo hayo," alieleza Mha. Lugodisha.

Alisema hatua inazochukua Mamlaka kututua changamoto hii kuwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa miundombinu na tathmini ya kupima mita zilizochakaa kwa maeneo ya Manispaa ambazo ufani wake umepungua na kuzibadilisha ili kuzuia mivujo.

"Tumefanya hivi ili kuhakikisha upatikanaji wa maji unaimarika na kwamba hii itachangia ukusanyaji wa mapato na kuwezesha kuwaunganishia wateja wapya huduma kwa gharama nafuu kwa kuwa mtandao utakuwa umeboreshwa," alieleza Mha. Lugodisha na kutoa wito kwa wadau wa maji kutunza miundombinu hiyo na kutoa taarifa kwenye Mamlaka watakapogundua kuna hujuma ya miundombinu kama vile kuiunganishia maji bila kufuata utaratibu ili sheria iweze kuchukua mkondo wake.

Miradi mikubwa ya maji mkoani Mtwara: Hatua kuelekea utekelezaji Kaulimbiu ya 'Kumtua Ndoo Mama Kichwani'



Na Emmanuel Chagu Paul, Mtwara

“Maji ni uhai.” Kauli hii inatokana na namna gani rasilimali ya maji ilivyo muhimu katika maisha ya viumbehai na binadamu. Maji hutumika kwa matumizi mbalimbali ikiwemo kilimo, kuendeshea mitambo viwandani, kuoga, kunywa, kupikia, kufua nguo na matumizi mengine mengi.

Sera ya maji ya 2002 kifungu cha 2 (1) – (12) kimebainisha matumizi mbalimbali ya maji. Katika kuhakikisha maji yanatumika kwa usahihii, Sheria ya Maji namba 5 ya mwaka 2019 imebainisha marufuku ya matumizi ya maji yasiyopangwa na imeweka adhabu mbalimbali kwa yejote mwenye kutumia maji kinyume na malengo yaliyokusudiwa.

Ili kuhakikisha maji yanapatikana kote mijini na vijijini, Sheria na Maji namba 5 ya 2019 imeanzisha vyombo vya kusimamia usambazaji wa maji vijijini na mijini, ambapo kifungu cha 9 cha Sheria hiyo kimeanzisha Mamlaka za Maji Mijini na kifungu cha 42 cha sheria hiyo kimeanzisha Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), yote hii ikiwa ni kuhakikisha huduma ya maji inapatikana katika maeneo ya mijini na vijijini.

EWURA CCC ikiwa ni chombo cha kuwakilisha na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji hufuatilia kwa karibu namna mamlaka za maji zinavyotekeleza majukumu yake, hususan kwa upande wa upatikanaji na uboreshaji wa huduma hizo.

Makala hii inajikita kwenye ubainishaji miradi mikubwa ya kimkakati ambayo imeanza kutekelezwa na Serikali ya Tanzania mkoani Mtwara ili kutekelezwa kaulimbiu ya “Kumtua ndoo mama kichwani.”

Kwa mujibu wa Kanali Ahmad Aba-

si Ahmad, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, iko miradi minne ya kimkakati ambayo imeshaanza kutekelezwa maeneo tofauti mkoani humo ambayo kufikia mwaka 2025 itakuwa imekamilika na kunufaisha watu zaidi ya milioni 1.6 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022. Baadhi ya miradi hiyo iliyoiezwa na Mkuu huyo wa mkoaa ni kama ifuatavyo:-

i. Ukarabati wa Miundombinu ya Mamlaka ya Majisafi ya Makonde

Miundombinu ya maji ya Makonde ilijengwa kabla ya uhuru wa Tanganika miaka ya 1950. Miundombinu hii imekuwa chakavu kiasi cha kushindwa kusambaza huduma inavyopaswa. Hata hivyo idadi ya wateja walio lengwa ilikuwa kidogo ukilinganisha na ongezeko la sasa ambalo ni zaidi ya watu laki 5.

Mradi wa ukarabati wa miundombinu ya maji Makonde wenye thamani ya milioni 84.7 utahusisha wilaya za Newala, Tandahimba na Halmashauri ya Nanyamba ambapo mkandarasi yuko eneo la kazi akiendelea na maboresho ya miundombinu hiyo. Kukamilika kwa uboreshaji huu mwaka 2025 kutanufaisha zaidi ya watu 552,985 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

ii. Mradi wa kutoa maji mto Ruvuma kwenda Mangaka (Nanyumbu)

Wilaya ya Nanyumbu ni moja ya wilaya ambazo zina upungufu mkubwa wa maji. Kuwepo kwa mradi huu kutiafungua Mangaka kiuchumi. Kiasi cha fedha cha shilingi bilioni 38.65 kimetengwa na Serikali na hivi sasa mkandarasi yuko eneo la mradi kwa utekelezaji. Mradi huo kufikia kukamilika kwake mwaka 2025 utanufaisa ha wakazi zaidi ya 204,323 wa eneo

hilo kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

iii. Uboreshaji wa Miundombinu ya Usambazaji wa Maji Manispaa ya Mtwara Mikindani

Serikali ya Tanzania imetenga fedha kiasi cha Shilingi bilioni 19.7 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji inayotumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara (MTUWASA) kusambaza maji mjini. Miundombinu hii ilijengwa zamani na ilikuwa imelenga kuhudumia watu wasiozidi elfu 50 tu ukilinganisha na ongezeko la sasa ambalo ni zaidi ya watu 146,772 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, ikiwa ni ongezeko la takribani asilimia 200 ya lengo la awali.

Upatikanaji wa maji katika Manispaa ya Mtwara umekuwa ni wa mgao kutokana na watu kunyang’anyana maji kwenye mtandao mdogo uliopo sasa. Mradi huu unategemewa kukamilika ifikapo mwaka 2025 na hivyo utakuwa umekidhi kauli mbiu ya Serikali ya kumtua ndoo mama kichwani. Mradi unatarajiwu kuongeza mtandao wa maji mpya wenye kilometra 45, hivyo kufanya watu Zaidi ya 140 watanufaika na mradi.

iv. Mradi wa Mnyawe hadi Nanyamba

Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 5.8 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kupeleka maji kutoka kijiji cha Mnyawe hadi Hal-mashauri ya Nanyamba ambapo zaidi ya watu laki moja na thelathini watanufaika na mradi huo.

Eneo la kutokea Mnyawe hadi Nanyamba halina mtandao wa maji kwa sasa na hivyo kukamilika kwa mtandao huu mpya utanufaisha vijiji vyote kwenye eneo hilo.

Kutekelezwa kwa miradi hii ya kimkakati kutapelekaa kupunguza changamoto za upatikananjaji wa huduma za maji kwa wananchi wa mkoaa wa Mtwara, na pia kutafungua mkoaa wa Mtwara kiuwekezaji na kuufanya mkoaa kuwa kimbilio la wawekezaji.

EWURA CCC inaendelea kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi hiyo ili kuhakikisha kuwa watumiaji wa huduma hiyo hatimaye wanapata huduma ya uhakika ya maji mkoani humo.

Makala

“**EWURA CCC ikiwa ni chombo cha kuwakilisha** na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji hufuatilia kwa karibu namna mamlaka za maji zinavyotekeleza majukumu yake, hususan kwa upande wa upatikanaji na uboreshaji wa huduma hizo.

Fahamu jinsi ya kusoma mita za maji pamoja na umuhimu wake

Na Amani Mbogo, Dodoma

Moya ya kazi kubwa inayofanywa na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) ni kutoa elimu kwa wananchi juu ya usomaji wa mita za maji kwa kuwa usomaji huo ndio hupelekeea mteja kupatiwa bili ya maji kwa mwezi husika kutokana na matumizi yake.

Mita ya maji ni kifaa kinachopima kiasi cha maji yanayotumiwa na mteja ambapo kwa kawaida huwekwa kwenye jengo la mteja na inaweza kuwa ya kidijitali au kimakanika.

Zipo faida nyingi kwa mtumiaji kujua usomaji wa mita za maji ikiwemo kufutililia kwa usahihi matumizi yake kwa kila mwezi. Hii inaweza kumsaidia mtumiaji kujua makadario yake ya bili pamoja na kutambua kama kuna mvujo wa maji baada ya mita. Mathalani endapo utaona mita yako inazunguka wakati hakuna matumizi ya maji, hiyo inaweza kuashiria kuwa kuna mvujo wa maji baada ya mita.

Kuangalia mita yako mara kwa mara ni njia rahisi ya kusaidia kuhifadhi maji na kuokoa fedha zako. Makala hii inakusudia kukuelimisha kujua namna ya kusoma mita za maji;

1. Kusoma mita za maji ya analogi

Mita ya analogi inaonesha sehemu mbili, ya kwanza ikiwa na nambari nyeusi ambayo huwakilisha kilolita (Lita1000/au mita moja ya ujazo) na pili ikiwa na nambari nyekundu ambayo inaonesha kiasi cha maji katika lita.

Ili kusoma mita yako anza kutoka kushoto kwenda kulia. Nambari nyeusi na nyeupe zinawakilisha kilolita (lita 1000) na nambari nyekundu zinawakilisha lita na pia kumbuka huhitaji kurekodi tarakimu (nyekundu) kwani bili kwa kawaida huhesabiwa kwa kila mita ya ujazo (kilolita) ya maji yanayotumika, na katika mita hizi bili ya maji ya mteja huwa inapatikana kwa kuangalia "units" alizotumia kwa mwezi husika kutoa "units" za mwezi uliopita ili kupata bili ya mwezi husika.

2. Kusoma mita ya maji ya digitali

Mita za maji za digitali ni mpya zaidi kuliko za analogi lakini zinafanya kazi kwa njia inayofanana. Mita ya digitali inakuwa na kioo kidogo au safu ya taa inayokuonesha ni kiasi gani cha maji ambacho umetumia. Hizi ni mita ambazo zinaendeshwa na betri na zinaweza kusambaza data kwa mbali kwa kisambaza maji.

Mita hizi ni za malipo ya kabla na kwamba mteja hununua kiasi cha maji kabla ya kuanza kutumia. Usomaji wa mita hizi mara nyingi huwa inaonesha kiasi cha pesa ulicholipia pamoja na lita ulizopewa na pindi lita zikiisha basi mita hii inajifunga.

Ni dhahiri kuwa uelewa wa jinsi ya kusoma mita za maji ni muhimu sana kwa watumiaji wa huduma hii. Kujuu kusoma mita za maji kunawezesha watumiaji kufutililia kwa usahihi matumizi yao, kutambua uvujaji wa maji, na hivyo kuokoa fedha zao.

EWURA CCC inalo jukumu kubwa katika kutoa elimu kuhusu usomaji wa mita hizi, ambayo ni kiini hasa cha kupokea bili za maji kwa matumizi ya mteja.




**JE UNATAARIFA,
MALALAMIKO AU
USHAURI KUHUSU
DUWASA?**

UNAWEZA KUWASILISHA
TAARIFA YAKO KUPITIA
MFUMO RAHSI WA
E-MREJESHO KIGANJANI
KWAKO

JINSI YA KUTUMA

- Piga*152*00#
- Kisha nenda no. 9
- Changua no. 2
- kisha fuata maelekezo

**KWA MSAADA ZAIDI
PIGA SIMU BURE
0800110078**


**MAMILAKA YA MAJISAFI NA USAFI
WA MAZINGIRA DODOMA (DUWASA)**

**MATUMIZI SAHIHI
YA MTANDAO WA
MAJITAKA**

**HAKIKISHA
UNAMWAGA MAJI
YA KUTOSHA**

**PIGA SIMU BURE
0800110078**

- Usitupe taka ngumu kwenye mtandao wa majitaka
- Usichepushie maji ya mvua kwenye mtandao wa majitaka
- Usiweke mchanga kwenye mtandao wa majitaka

Mtumiaji

• Toleo Na. 09 • Januari - Juni, 2024

uk. 24

Baraza lashiriki utatuzi lalamiko lililodumu kwa miaka miwili

Na Dennis Ndanu, Mara

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kupitia Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Mara imefanikiwa kutatta mgogoro uliodumu kwa zaidi ya miaka miwili baina ya TANESCO na Ndugu Asa Meena, aliyekuwa analalamikia nguzo ya umeme kuwekwa katika kiwanja chake hivyo kushindwa kukiendeleza kiwanja hicho.

Meena amelilalamikia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kusimika nguzo ya umeme katika kiwanja chake namba 87 Block "T" mtaa wa Mwisenge kata ya Mwisenge Manispaa ya Musoma na hivyo kusababisha ndugu Meena kushindwa kuendeleza ujenzi wa makazi yake katika kiwanja hicho.

Akiwasilisha lalamiko lake katika ofisi ya EWURA CCC Mara, Meena alisema "nilifuatilia suala hili mara nyingi katika ofisi za TANESCO na kupewa watu tofauti tofauti wa

kushughulikia lalamiko langu, lakini sijapata mafankio yoyote. Niliandika barua kwenda TANESCO zaidi ya mara mbili lakini hazijajibowi, mwisho niliamua kumuona Afisa Mpango Miji wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ambaye alinieleza kuwa kawaida nguzo za umeme, simu na mabomba ya maji hujengwa kwenye hifadhi ya barabara."

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Mara baada ya kulipokea lalamiko la mteja huyo iliamua kuanzisha mazungumzo ya kutafuta muafaka baina ya TANESCO na ndugu Meena.

Katika kikao cha pamoja baina ya TANESCO, Ndungu Meena na Kamati ya Watumiaji makubaliano yalifikiwa kwamba TANESCO wandonoe nguzo hiyo ndani ya kipindi cha muda wa mwezi mmoja, kwani kiwanja hicho ni mali halali ya ndugu Meena.

Baada ya kikao hicho ndugu Meena aliishukuru EWURA CCC kwa msaada aliopatiwa wa kutatta mgogoro baina yake na TANESCO, mgogoro ambao ulidumu kwa zaidi

ya miaka miwili.

"Naishukuru sana EWURA CCC kwani ndani ya mwezi mmoja tu lalamiko langu limetatuliwa. Nawasihi muendelee kufuatilia changamoto za watumiaji wengine wa huduma za nishati na maji kwani ni nyingi sana na wananchi wengi hawajui wapi wapeleke malalamiko yao pamoja na changamoto wanazopitia," alisema ndugu Meena.

Kwa upande wake Bw. Robinson Wangaso ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Mara alizipongeza pande zote mbili kwa makubaliano waliyofikia pasipo ugumu wowote.

"TANESCO na ndugu Meena mmeonesha ukomavu katika jambo hili, kwani limetatuliwa bila mabisano. Kwa pande zote kuafikiana imewezesha mtumiaji Ndg. Meena kupata haki yake, kadhalika TANESCO mmetimiza wajibu wenu kwa mwananchi huyu ambaye pia ni mteja wenu mtarajiwa pindi atakapokutwa amekamilisha ujenzi wake katika kiwanja chake," alisema Wangaso.

Ushauri

MUWASA

SABABU ZA BILI YA MAJI KUWA KUBWA

Kama unahisi bila yako ya maji ni kubwa kuliko unavotumia. Fuata njia rahisi zifuatato kujua chanzo.

- 1 Funga koki zote za maji
- 2 Angalia mita yako kama bado inazunguka
- 3 Subiri kwa muda wa nusu saa na angalia tena kama mita inazunguka

Matokeo
Ikiwa mita itaeonekana ikizunguka basi ni ishara kuwa kuna mivujo midogo kwenye maungio ya mabomba ya maji

Tufuutilie [muwasamusoma](#)

ELIMU ZAIDI: 0800110108 (BURE)

MUWASA

GHARAMA ZA MATUMIZI YA MAJI KULINGANA NA KUNDI LA MTEJA



KUNDIA - WATEJA WA MAJUMBANI (DOMESTIC)	
UNITS	BEI (Tshs.)
1→5	1040.00
6→10	1210.00
10→KUENDELEA	1330.00

UNITS	BEI (Tshs.)
(kuanza 1→5)	5 * 1040 = 5200
(kuanza 6→10)	2 * 1210 = 2420
jumla ya unit	7620.00
Ewura fee (1% ya jumla)	76.20
JUMLA YA ANKARA (jumla+ewura)	7696.20



[muwasamusoma](#) [08001101108](#)

HabariPicha



Bi. Chipegwa Samwel, Afisa Msaидизи Huduma kwa Wateja na Utawala, EWURA CCC Morogoro akitoa elimu kwa baadhi ya wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi Mlimani kuhusu changamoto zinazowakabili watumiaji wa huduma za nishati na maji na namna ya kuziwasilisha kwa watoa huduma. Picha zote na Mpigapicha Wetu



Bi. Sakina Yusuph, Afisa Msaيدизи Huduma kwa Wateja na Utawala, EWURA CCC Tabora akitoa elimu kuhusu haki na wajibu wa mtumiaji wa huduma za nishati na maji kupitia kituo cha Redio cha TAA Bora FM kilichopö katika Manispaa ya Tabora.



Mmoja wa washiriki wa semina kuelekea kilele cha Maadhimisho ya "Siku ya Mtumiaji Duniani 2023" akichangia mada zilizowasilishwa na Baraza. Pamoja na wadau wengine, semina hiyo iliwakutanisha wanafunzi wa shule za sekondari na vyuo vikuu jijini Mwanza chini ya uratibu wa Jukwaa la Watumiaji Tanzania (Tanzania Consumer Forum).

HabariPicha



Mhe. Exaudi S. Kigahe, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara akitoa maelekezo kwa Baraza kufikisha elimu kwa watumiaji wengi zaidi wa huduma za nishati na maji alipotembelea banda la EWURA CCC wakati wa Maonesho ya kitaifa ya Nanenane 2023 yaliyofanyika jijini Mbeya kwenye Viwanja vya Mwakangale.



Ndugu Lugiko L. Lugiko, Kaimu Afisa Uelimishaji na Uhamasishaji, EWURA CCC akitoa elimu kupitia vyombo vya habari, pamoja na mambo mengine kuhusu kazi za Baraza wakati wa maonesho ya kitaifa ya Nanenane 2023 yaliyofanyika jijini Mbeya kwenye Viwanja vya Mwakangale.



Wadau mbali mbali wakiwa katika banda la EWURA CCC wakipata elimu na kusaini kitabu cha wagensi wakati wa Maonesho ya Nanenane 2023.



Vifaa vya umeme ambavyo ni mali ya Shirika la Ugavi Umeme Tanzania (TANESCO) vikiwa vimekamatwa na Jeshi la Polisi kutoka mikononi mwa wahujumu wa mindombinu ya Umeme. Picha kwa hisani ya Malunde blog

Wajibu wa mtumiaji katika kuleta ufanisi, ubora wa huduma

Na Geofrey Sokesia, Singida

Matumiaji wa huduma za nishati na maji ni mtu ye yote, taasisi au kam-puni yoyote inayotumia huduma au bidhaa zinazodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwa matumizi binafsi na siyo kufanya biashara. Huduma hizi zinajumuisha nishati kama vile umeme, mafuta, gesi pamoja na huduma za maji yanayotolewa na mamlaka za maji nchini.

Katika kutumia huduma hizi baadhi ya watumiaji wamekuwa wakipata changamoto mbalimbali zikiwemo kupewa bili zisizoendana na matumizi yao halisi hasa watumiaji wa maji, kukatiwa huduma bila taarifa, usomaji wa mita za maji

usio sahihi, kupata huduma isiyi na kiwango bora, majibu mabaya kuto-ka kwa watoa huduma, uchelewe-shaji wa maunganisho mapya ya huduma pamoja na hasara zin-azoweza kutokana na huduma hizi.

Ili kupunguza changamoto hizi watumiaji wanatakiwa kuwa seh-emu ya utatuza wake kwa kushirikiana na watoa huduma na hivyo kufanya watumiaji kufurahia huduma badala ya kuzichukia.

Watumiaji wanao mchango mkubwa sana katika kuboresha up- atikanaji na utoaji wa huduma hizi. Ili mchango wao uonekane ni lazima watekeleze wajibu wao kama inayoelezwa katika makala hii:-

i. Kulalamikia huduma mbovu

Kanuni ya 61(1-6) ya Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi

wa Mazingira (Ubora wa Huduma na Leseni) za Mwaka 2020; Tangazo la Serikali Na. 849 zinaonesha utaratibu wa mtoa huduma kushughulikia malalamiko ya wateja wake. Hii ni fursa muhimu inayotolewa na sheria ili watumiaji waeleze changamoto zao ili kupata utatuza na uboreshaji wa huduma husika. Kulalamika hu-susani kwa maandishi kutasaidia kuweka kumbukumbu za lalamiko lakini pia hiyo itamfanya mtoa huduma kuwajibika. Watumiaji wakikaa kimya bila kulalamikia huduma mb-ovu watoa huduma wanaweza kub-weteka na kuemdee kutoa huduma pasipo kujali viwango bora vya huduma vilivyowekwa.

ii. Kutoa taarifa

Mkataba wa Huduma kwa Mte- ja wa TANESCO kipengele D(2)(d)

kinaeleza kuwa moja ya wajibu wa mtumiaji wa huduma ya umeme ni pamoa na kutoa taarifa kwa Shirika. Taarifa hiyo inaweza kuhusu uharibifu wa miundombinu, mteja kuhama nyumba, au kuhusu hatari zitokanazo na huduma ya umeme kama vile majanga ya moto, wizi wa huduma ya umeme, lakini kwa upande wa huduma ya maji mtumiaji ana wajibu wa kutoa taarifa juu ya bomba la maji kupasuka au huduma ya maji kukosekana. Watumiaji wanatakiwa kutoa taarifa kwa mtoe huduma husika kwani itasaidia utatuzi wa changamoto husika kwa haraka.

iii. Kutafuta taarifa na kuongezza maarifa juu ya bidhaa za nishati na maji

Katika kuboresha huduma za nishati na maji ni muhimu watumiaji kujijengea utamaduni wa kutafuta taarifa au elimu kuhusu huduma hizi. Kwa kufanya hivyo itawaongezea uelewa wa haki na wajibu wao. Watumiaji kuwa na maarifa au taarifa sahihi kutawapa ujasiri wa kuhoji au kuwakosoa watoe huduma pale wanaposhindwa kutoa huduma kwa uhakika, ubora na kwa utaratibu uliowekwa. Taarifa au maarifa hayo yanaweza kupatikana kwa kusoma

machapisho mbalimbali vikiwemo vitabu.

iv. Kulipia huduma uliyotumia Kanuni ya 51(1) ya Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira (Ubora wa Huduma na Leseni) za Mwaka 2020 inamta-ka mteja wa huduma za maji kulipa bili yake ndani ya siku 30 tangu ali-pookeka.

Sambamba na hilo, Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa TANESCO kipengele D(2)(a) kinaeleza kuwa wajibu wa mteja wa umeme ni kulipia kwa wakati gharama za umeme alizotumia. Ifahamike kuwa taasisi zinazotoa huduma za nishati na maji huijidesha kutokana na mapato wanayokusanya kutoka kwa wateja wao, na kuititia makusanyo hayo huweza kuboresha au kuongeza mtandao wa upatikanaji wa huduma hizo. Kwa kuzingatia ukweli huu ni wazi kwamba watumiaji wote wana wajibu wa kulipia bili za matumizi ya huduma hizo kwa wakati.

v. Kufichua wahujumu na kulinda miundombinu

Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida kipengele 6.2 kinaeleza kuwa mtumiaji wa hudu-

ma ya maji ana wajibu wa kutohuju-mu miundombinu au huduma kama vile wizi wa mita au kuchepusha huduma kwa lengo la kukwepa bili. Vitendo vya namna hii vinapelekeea si tu mtoe huduma kupata hasara na kushindwa kabisa kuijidesha bali pia vinawakosesha watumiaji wengine kupata huduma hizo za msingi.

Pia Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa TANESCO kipengele D(2)(b) kinaeleza kuwa wajibu mojawapo wa mteja wa umeme ni kulinda mali za TANESCO zilizopo kwenye maeneo yake ili kuwepo na uendelevu wa huduma hizo. Wahujumu wasipofichuliwa ni dhahiri kuwa Serikali itakwamishwa katika jithiada zake za kuwapatia Watanzania huduma za nishati na maji zilizo bora na za uhakika.

Watumiaji wa huduma za nishati na maji kwa ujumla kama watatekeleza vizuri wajibu wao hususani katika ulipaji wa bili kwa wakati, kufichua wahujumu miundombinu, kulalamikia huduma mbovu pamoa na kushiriki au kutoa maoni juu ya huduma za nishati na maji basi hii itapelekeea huduma kuwa bora na endelevu kwa sasa na vizazi vi-javyo.


WIZARA YA MAJI
 MAMLAKA YA MAJISAFI NA
 USAFI WA MAZINGIRA SINGIDA (SUWASA)

LIPA KWA SIMU


**JE UMESHALIPA
BILI YAKO?**

UNASUBIRI NINI?

LIPA KWA BENKI


 Ni wajibu wako mteja kulipa bili yako ya kila mwezi bila kulaza,
 Unapolipa bili yako kwa wakati unaiwezesha SUWASA kukupatia
 huduma iliyo bora zaidi na endelevu
 Ikiwa haujapata bili yako ya mwezi Juni
 piga simu namba
0800710038
#epukauzumbu

 [suwasa.singida](#)
 [Suwasa Singida](#)  Bure 0800710038  [www.suwasa.or.tz](#)

WIZARA YA MAJI
 MAMLAKA YA MAJISAFI NA
 USAFI WA MAZINGIRA SINGIDA (SUWASA)

**UTARATIBU WA KUPATA HUDUMA
YA MAJI (MAUNGANISHO MAPYA)**

- 1. Mteja atajaza fomu ya maunganisho mapya.**
- 2. Mteja analakiwa kuwa na nakala za nyaraka zifuratazo:**
 - Picha (Passport size) au
 - Iseeni ya udereva au
 - Kitambulisho cha Taifa au
 - Ramani ya makazi au
 - Kitambulisho cha kupigia kura au pasipoti ya kusafiria
- 3. Ikiwa mteja hana ramani ya makazi alete barua kutoka kwa mwenyekiti wa mtaa.**
- 4. Mteja atatembelewa na maafisa wa SUWASA kufanyiwa tathmini ya gharama.**
- 5. Mteja atatumiwa namba za malipo ya maunganisho**

Mara baada ya malipo mteja ataunganishiwa huduma ndani ya siku 7. #kaziendelee

 [suwasa_singida](#)
 [Suwasa Singida](#)  Bure 0800710038  [www.suwasa.or.tz](#)

Huu ndio utaratibu maalum kugharamia miundombinu ya umeme

Na Emmanuel Paul, Mtwara

Umeme ni nishati muhimu sana kwa maendeleo ambayo hurahisisha utendaji wa kazi za binadamu ambapo matumizi yake yameenea katika maeneo mbalimbali ikiwemo viwanda, sehemu za biashara na majumbani.

Sehemu nyingi duniani huduma za umeme husambazwa na kampuni zilizopewa dhamana na serikali. Katika nchi yetu Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ndio Shirika lilopewa dhamana hiyo ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme kwa watumiaji wa nishati hiyo.

Mbali na TANESCO kuna kampuni zingine ndogondogo kama vile Mwenga Power Service Limited ambapo imepewa leseni na Mamlaika ya Udhibiti wa huduma za Nishati na Maji (EWURA) kusambaza umeme maeneo ya Mufindi mkoani Iringa.

Katika kutekeleza shughuli ya usambazaji wa umeme, Shirika au Kampuni yenye dhamana hiyo hutumia laini za kusambaza umeme kwa mujibu wa Mwongozo wa Wahandisi wa Umeme wa 2004 toleo

la 9 unaonesha aina za laini za usambazaji.

Makala hii inajikita kujadili utaratibu wa kugharamia laini za umeme zinazotumika kufikisha huduma ya umeme kwa mteja ambazo ni laini ya umeme ya huduma (service line) na laini ya usambazaji (distribution mains). Laini hizi ndizo zinazotumika kumfikishia mteja huduma ya umeme.

Laini pia zimeoneshwa kwenye Sheria ya Umeme 2008 na marekebisho yake namba 3 ya 2020, Kanuni za Umeme za Jumla za 2020 na Mwongozo wa Wahandisi wa TANESCO wa 2004 toleo la 9.

i. Laini ya Usambazaji (Distribution Main)

Hihi ni njia ya umeme inayojengwa na aliyepewa leseni ili kusogezwa huduma kwa wahitaji. Njia hii ya umeme hujengwa kutoka kwenye transfoma kuelekea kwa wahitaji wa umeme. Kwa mujibu wa Sheria ya Umeme ya Mwaka 2008, njia hii inatakiwa kugharimiwa na msambazaji aliyepewa leseni ya kazi hiyo. Lakini pia ifahamike kuwa ikitokea miundombinu ya umeme hajafika umbali wa mita 30 toka lilipo eneo la mteja na TANESCO ikawa haina uwezo wakati huo wa kujenga laini

ya usambazaji, basi mteja anawenza kuamua kugharamia ujenzi wa laini hiyo.

Na kwa mujibu wa Kanuni ya 4(1) na (2) ya Kanuni za Umeme za Jumla za mwaka 2020 mteja ataka-yeamua kujengwa laini ya kusambaza umeme atarejeshewa fedha zake kwa kupewa punguzo la asilimia 40 kwa kila bili zake za mwezi hadi gharama zake alizozitumia kwenye ujenzi zirudi.

ii. Laini ya Huduma (Service Line)

Njia hii ya umeme ndiyo njia ambayo mteja anatakiwa kuchangia gharama za ujenzi, ambapo sheria na kanuni zimewaka viwango vya umbali utakaogharimiwa na mtu anayehitaji huduma ya umeme.

Viwango vya umbali wa laini ya huduma vimeoneshwa kuwa ni viwili tu ambapo kimoja ni cha jumla na kingine kinatokea endapo kuna sababu maalumu hasa kwa maeneo ya vijiji.

Umbali uliokubalika ni mita 30 kutokea kwenye miundombinu ya TANESCO ilipokomea. Umbali huu ndiyo mteja anayeomba umeme atatakiwa kuulipia. Kifungu cha 4.3.13 cha Mwongozo wa Wahandisi wa TANESCO kinalezea kuwa kwa mazingira yasiyoziulika vijiji, umbali wa laini ya huduma unaweza ukaongezeka bila kuzidi mita 50 kutoka ule wa awali uliowekwa wa mita 30.

Kwa mujibu wa Agizo la Bei za Umeme (Tariff Order) za TANESCO la EWURA la mwaka 2016 na marekebisho yake ya Mwaka 2020 mteja anayeomba umeme TANESCO anawajibika kulipia gharama za laini ya huduma. Kwa mantiki hiyo urefu wa laini ya huduma ni ongezeko la gharama kwa mteja anayeomba huduma ya umeme. Serikali ya Tanzania kwa kuliona hilo imewe kwa viwango vya umbali ambavyo mteja anayeomba huduma ya umeme atatakiwa kugharamia.

TANESCO inahimizwa kwa mujibu wa sheria za umeme na kanuni zake kuhakikisha inatekeleza wajibu wake wa kufikisha miundombinu ya umeme ndani ya mita 30 ili kumpunguzia gharama mteja anayehitaji huduma ya umeme.



Moja ya laini ya huduma (service line) inayotumika kupeleka huduma ya umeme kwenye nyumba ya mteja. Picha na Mpigapicha Wetu

Hatimaye nimepata mita mpya - Mtumiaji

Na Mwandishi wetu, Iringa

Matumiaji wa huduma za nishati na maji Bi. Saida Seuguli ambaye ni mkazi wa Zizi Vitindini Mkoa wa Iringa amelishukuru Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoani humo kwa kumsaidia kubadilishiwa mita yake ya maji iliyokuwa imechakaa kwa muda mrefu.

Akitoa ushuhuda wake katika ofisi za EWURA CCC, Bi. Seuguli alisema kuwa mwanzo wa kupata msaada wake ni pindi alipotembelea banda la EWURA CCC kuitia Maonesho ambapo Baraza lilimuelimisha kuhusu haki na wajibu wake kama mtumiaji wa huduma za nishati na maji na hatimaye kumsaidia katika utatuza wa changamoto yake. Bi. Saida alisema kuwa Baraza limemsaidia kufuatilia na kushughulikia tatizo lake hilo la muda mrefu la uchakavu wa mita ambapo kioo chake kilifikia hatua ya kutoonesha namba zozote.

"Ni kwa muda sasa mita yangu ya maji ilikuwa imechakaa sana na nilikuwa nimeshatoa taarifa kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA) lakini haikubadilishiwa. Baada ya kusikia kuna maonesho nilitembelea mabanda mbalimbali nikiamini naweza kupata msaada kutoka taasisi mbalimbali mbazo huja kutoa elimu kwenye maonesho, na ndipo nilipofika katika banda la EWURA CCC nikawasilisha tatizo langu," alieleza Saida na kuongeza kuwa EWURA CCC ilipokea lalamiko lake na kuahidi kufuatilia utatuza wake.

Bi. Seuguli alitoa ushuhuda akisema "Ninashukuru mita yangu sasa imebadilishwa na hivyo changamoto yangu ya muda mrefu imeisha. Nalishukuru sana Baraza kwa kunisaidia kupata huduma hiyo," alisema Bi. Seuguli.

Awali baada ya kupokea lalamiko la mteja, EWURA CCC Iringa ilifuatilia lalamiko hilo na kuliwasilisha IRUWASA na hatimaye kutatuliwa.

Akizungumza wakati alipofikishiwa lalamiko hilo ofisini kweke Bi. Restuta Sakila ambaye ni Afisa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliiano na Mahusiano kwa Umma wa IRUWASA alisema "Ni kweli mita ya mteja wetu ilikuwa na changamoto na IRUWASA italifanya kazi ili mteja apate mita nyngine."

EWURA CCC mkoani Iringa kuitia kwa Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala Bi. Brenda Magoma alisema pamoja na lalamko hili la mteja, Baraza katika kutimiza majukumu yake bado litaendelea kutoa elimu kwa watumiaji juu ya haki na wajibu wao lengo likiwa ni kuwajengea uwezo wa kujua haki na wajibu wao ili hatimaye waweze kuzikabili changamoto zitokanazo na huduma za nishati na maji.

"Katika kuwaflikia watumiaji hao, tutatumia fursa mbalimbali yakiwemo maonesho pindi yanapojitokeza katika mkoaa wetu ili tuwafikie wananchi wengi zaidi," alisema Bi. Magoma.

Alisitisiza kuwa Baraza litaendelea kutoa elimu kwa kutumia majukwaa mbalimbali yatakayojitokeza ndani ya Mkoa wa Iringa ili wananchi waweze kufahamu haki na wajibu wao kuhusu huduma za nishati na maji.

Uwajibikaji



WIZARA YA MAJI
MAMILAKA YA MAJISAFI NA USAFI
WA MAZINGIRA IRINGA (IRUWASA)



HAKIKI USOMAJI WA MITA YAKO

Ndugu mteja hakikisha unashiriki zoezi usomaji wa mita ya maji mara upatapo ujumbe mfupi kuhusu usomaji wa mita yako. Endapo utakuta kuna tofauti pigi bure simu: 0800110122.



0800 110 122 | @iruwa.sa | @Iruwasa Iringa



WIZARA YA MAJI
MAMILAKA YA MAJISAFI NA USAFI
WA MAZINGIRA IRINGA (IRUWASA)





**Je Unahitaji Huduma
ya Kuondolewa Majitaka ?**

Hujachelewa IRUWASA inatao huduma hii kwa wananchi, Taasisi za serikali na binafsi kwa gharama nafuu

0800 110 122 | @iruwa.sa | @Iruwasa Iringa

Baraza lamsaidia Bi. Mwamvua kulipwa fidia

Na Mwandishi wetu, Tanga

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoani Tanga limemsadia Bi. Mwamvua Maliki mkazi wa Mwamboni Tanga kulipwa fidia ya kiasi cha shilingi 778,000/= kutokana na kuunguliwa vifaa vyake nya umeme ndani ya nyumba yake baada ya waya wa umeme kudondokea paa la nyumba yake mnamo tarehe 31/08/2022.

Bi. Mwamvua amebainisha kuwa alipata msaada kupitia kipindi cha redio kinachendeshwa na EWURA CCC juu ya haki za mteja na fidia zinazotolewa kwa mteja mwenye changamoto juu ya huduma za nishati na maji na ndipo alipoamua kuchukua hatua za kuanza kudai fidia.

"Mara baada ya kusikiliza kipindi cha redio nilipata mawasiliano ya ofisi ya EWURA

CCC na kufika ofisini kwao ndipo waliponisaidia kujaza fomu ya malalamiko na baada ya hapo niliitwa kwenye kikao cha Usuluhishi na EWURA pamoja na watu wa TANESCO kwa lengo la kutafuta muafaka wa shauri langu," alisema Bi. Mwamvua.

Kwa upande wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kupitia Afisa Huduma kwa Wateja Kanda ya Kaskazini Bi. Evelyn Shundi alikiri kupokea malalamiko hayo ya kutafuta muafaka, na katika kikao hicho TANESCO iliagizwa kulipa kiasi cha shilingi 778,000/= kama fidia ya vifaa nya mteja huyo ambavyo vilungua kutokana na hitilafu hiyo ya umeme.

Akiongea baada ya kikao cha usuluhishi Bi. Shundi alikiri kuwa EWURA ilipokea malalamiko ya mteja kutoka EWURA CCC na kupitia kikao cha usuluhishi cha tarehe 14/02/2023 EWURA iliagiza TANESCO

kumlipa mteja fidia ya hasara aliyoipata ya kuunguliwa vifaa vyake nya umeme.

Naye Bi. Nuru Zuberi Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala EWURA CCC Mkoa wa Tanga aliahidi kuendela kutoa elimu kwa umma ili watumiaji wengi wa huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA wapate uelewa zaidi wa haki na wajibu wao.

"Ni moja ya wajibu wa Baraza kutoa elimu mara kwa mara kwa umma ili kuhakikisha wananchi wanaelimika na kutambua haki na wajibu wao, ikiwemo kudai fidia pindi wanapopata hasara au athari zitokanazo na huduma zinazodhibitiwa na EWURA," alisema Bi. Zuberi na kuongeza kuwa njia mojawapo inazotumia EWURA CCC kutoa elimu ni kupitia vyombo nya habari kama vile redio, televiseni, mitandao ya kijamii na hata katika mikutano mbalimbali ya hadhara.


WEEKEND NJEMA
Endelea kufurahia huduma za TANGA UWASA popote ulipo na kwa wakati wowote.

- Fanya malipo ya huduma kwa urahisi na uharaka kwa kutumia simu yako ya mkononi.
- Wasiliana nasi kwa taarifa, elimu na huduma.
- Pata taarifa na elimu sahihi juu ya huduma za TANGA UWASA.

Tigo Pesa *150*01# **Vodacom m-Pesa** *150*00# **haloPesa** *150*88# **Airtel** *150*60# **PESA** *150*71#

0735 800 111 **0800 110 111** Piga simu **BURE**

TangaUwasa     

"Kila Tone Lina Thamani"


KUWA MZALENDÖ, LIPIA BILI YAKO SASA
Ndugu mteja, Anza mwezi Kizalendo kwa kufanya malipo ya bili kwa wakati ili kuwezesha utoaji wa huduma bora na endelevu.
Fanya Malipo sasa kwa urahisi na uharaka kupitia

LIPA KWA NJIA YA SIMU	BENKI WASHIRIKA
tigo pesa *150*01# m-Pesa	NMB
haloPesa *150*88# airtel money	C&B BANK
T-Pesa	NBC National Bank of Commerce

TangaUwasa     

0735 800 111 **0800 110 111** **BURE**

"Kila Tone Lina Thamani"

Je, wamfahamu mteja muhimu wa TANESCO?

Na Neema Nkoko, Manyara

Watumiaji wa umeme wa TANESCO wanaweza kugawanya-wa katika makundi mbalimbali ikiwemo watumiaji wa majumbani, hoteli, taasisi, viwanda na kadhalika, lakini pia aina nyingine ya kuwabaini watumiaji wa TANESCO ni kwa kuangalia kiasi cha umeme wanaotumia kwa mwezi.

Makala hii inalenga kuonesha watumiaji wanaotajwa kama wateja muhimu wa TANESCO ambapo itaangazia sifa za uteuzi wa kuwa mteja muhimu na haki za aina hii ya wateja, lengo likiwa ni kuwa ongezea ulewa wasomaji pindi wanapohitaji kuwa kwenye kundi hili la wateja muhimu. Rejea mbalimbali kwenye Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Upelkaji na Usambazaji

Umeme za Mwaka 2023 zilizochapishwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 452 zitatumika katika kufafanua juu ya jambo hili.

Vigezo vyta uteuzi wa mteja muhimu vimeainishwa na Kanuni ya 75 (1) ya Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Upelkaji na Usambazaji Umeme kama ifuatavyo;

(a) Mwombaji awe anapata umeme wenye nguvu si chini ya 33kv;

(b) Mwombaji awe na mahitaji ya umeme wa kiwango cha juu cha megawati mbili au zaidi; na

(c) Kama mwombaji anapelekewa umeme na mwenye leseni ya usambazaji, anatakiwa kupata barua ya kuthibitisha hayo kutoka kwa mwenye leseni ya usambazaji ili kuihakikishia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kuwa hakuna madai yoyote na hadai chochote.

Kanuni ya 75(2) ya Kanuni tajwa inasitiza kuwa bila kujali masharti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha Kanuni hizo, EWURA inaweza kukubali ombi la kuwa mteja muhimu pasipo mteja kufikia viwango husika kama hali inaruhusu kufanya hiyo.

Haki anazopewa mteja muhimu wa umeme

Haki za mteja muhimu zimeelezwa kwenye Kanuni ya 77 ya Kanuni tajwa hapo juu kuwa mteja yeyote anayepewa wadhiifa wa kuwa mteja muhimu na EWURA atakuwa na haki zifuatazo:-

(a) Kununua umeme kuto-ka kwa mwenye leseni ya kuzalisha umeme anaye mtaka yeye;

(b) Kuingia mkataba wa ununuzi wa umeme na mwenye leseni ya kuzalisha umeme pasipo kuomba idhini ya EWURA; na

(c) Kuingia katika majadiliano ya bei ya umeme kuzingatia uelewano uliopo na muuzaji umeme.

Kwa kuzingatia vigezo hivyo mteja yeyote mwenye vigezo hivyo anaweza kuwasilisha maombi yake EWURA ya kuwa mteja muhimu na pengine akapata huduma stahiki kulin-gana na mahitaji yake ya umeme.

Makala


**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
MWANZA (MWAUWASA)**



**PATA TAARIFA SAHIHI YA HUDUMA ZA MWAUWASA
KUPITIA MITANDAO YETU YA KIJAMII**

0800110023
Huduma Kwa Wateja

Mwauwasatz
Instagram

Mwauwasa
Facebook

www.mwauwasa.go.tz
Website

Mwauwasatz
Twitter

0800110023 (Bure) | www.mwauwasa.go.tz | [Mwauwasa](#) | [Mwauwasatz](#)


**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
MWANZA (MWAUWASA)**



**HUDUMA YA UONDOSHAJI WA
MAJITAKA MAJUMBANI**

MWAUWASA inatoa huduma ya kuondosha majitaka majumbani kwa gharama nafuu.

Wasiliana nasi kupitia namba **0800110023 (BURE)**.

0800110023 (Bure) | www.mwauwasa.go.tz | [Mwauwasa](#) | [Mwauwasatz](#)

SOUWASA: Hizi ndizo hatua za kutibu maji kabla ya kwenda kwa mtumiaji

Na Magreth Temba, Ruvuma

Katika kutekeleza majukumu yake ofisi ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) Mkoa wa Ruvuma imekuwa ikitembelea makundi mbalimbali ya wananchi na kuwapatio elimu kuhusu haki na wajibu wao kama watumiaji wa huduma za nishati na maji.

Kupitia majukwaa hayo ya kutoa elimu, EWURA CCC imekuwa ikipokea na kuyafanyia kazi maswali na kero mbalimbali zinazohusu huduma za nishati na maji.

Miongoni mwa kero au maswali ambayo yamekuwa yakiulizwa mara kwa mara ni pamoja na wananchi kuwa na wasiwasi na maji wanayotumia toka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA) kutotiba vizuri kwa kuwa kuna nyakati wanapata maji yenye vumbi hivyo watumiaji kuhisi kuwa maji hayo si salama.

Makala hii inalenga kutoa elimu juu ya hatua zinazofanya na kuzingatiwa na SOUWASA katika kutibu maji kabla hayajawafikia watumiaji. Mhandisi Jafari Yahaya ambaye ni Kaimu Mkurugenzi wa Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira (SOUWASA) anaeleza kuwa Mamlaka zote za Majisafi na Usafi wa Mazingira

zimekuwa zikifanya hatua zifuatazo katika kuyatibu maji kabla ya kuwafikia watumiaji:

1. Utoaji madini Chuma na Manganisi

Hii ni hatua ya kutoa madini aina ya Chuma na Manganisi ambayo hayatakiwi kuwepo kwenye maji yanayotumiwa na binadamu kwa sabbu yanaweza kuleta athari za kiafya, hasa kwa watoto na akina mama wajawazito.

2. Utoaji mchanga na tope

Hii ni kuondoa mchanga na tope kwenye maji. Vitu hivi vikishajitenga maji hubaki safi ambapo mchanga unajitenga mahali pake na tope nalo linajitenga mahali pake ili kuruhusu maji kubaki safi na kwenda kwenye hatua nyingine ya usafishaji.

3. Uwekaji Dawa

Katika hatua hii maji huwekwa dawa aina ya Shabo; kazi ya dawa hii ni kuhakikisha tope lote limeyeyuka kwenye maji na kuondoa vumbi.

4. Ukusanyaji vumbi

Hatua hii kitaalamu huitwa "floatation." Hatua hii ni kwa ajili ya kukusanya vumbivumbi lote lililopo kwenye maji na kutengeneza mabonge na kukusanya mabonge yote kwenda kwenye chujio kwa ajili ya

kutengeneza njia na maji kupita.

5. Uchujaji maji

Hii ni moja ya hatua muhimu sana katika kutibu maji kabla ya kumfikia mtumiaji kwani hapa ndipo hatua ya kuondoa mabonge yote ya vumbivumbi na michanga hufanyika. Chujio la maji huruhusu maji yaliyo safi tu kuweza kupita kwa ajili ya kwenda kutibiwa kabla ya kuruhusiwa kutiliwa na wateja.

6. Uwekaji dawa Chlorine

Hii ni hatua ya kutibu maji kabla hayajaenda kwa watumiaji ambaipo maji huwekwa dawa aina ya chlorine. Dawa hii inasaidia kuua wadudu na bacteria wanaowenza kusababisha magonjwa kwa binadamu yanayotokana na maji na pia husaidia kuweka ulinzi kwenye maji kwa kuzuia athari zozote za maradhi kwa watumiaji.

Kwa kuzingatia kanuni hizi za usalama za kutibu maji, dhamira ya SOUWASA inakuwa imetimia katika kutoa maji salama na bora kwa jamii na hivyo kudumisha afya na ustawi wa wananchi wa mkoa wa Ruvuma.

Baraza linaamini kuwa elimu hii iliyofafanua kwa kina hatua zinazochukuliwa na SOUWASA ni ya muhimu kwa watumiaji wote wa maji.

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SONGEA (SOUWASA)

ANZA WIKI KWA KUPATA HUDUMA BORA KUTOKA SOUWASA

Kwa changamoto yoyote, kutoa maoni, wasiliana nasi kupitia namba:

0800 110010
067 7091360

au tembele mitanadao yetu ya kijamii kwa jina la SOUWASA

Piga simu Bure 0800 110010/0677091360

Souwasa

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SONGEA (SOUWASA)

Je umeshalipa? Bili Yako

Lipia sasa ankara yako kupitia Mitandao ya simu pamoja na Benki washirika na App ya GePG. Ili kuepuwa usumbuwa wa kukatiwa/kusitishiwa huduma ya maji.

NMB
COB BANK
NBNC
GePG

tigo pesa
m-pesa
halo pesa
airtel money
T-PESA

Piga simu Bure 0800 110010/0677091360

"SOUWASA huduma bora kwa wote"



Bi. Zamda Mabada (kulia), Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala, EWURA CCC Kilimanjaro, akitoa elimu kuhusu huduma za nishati na maji kwa mwananchi aliyetembelea banda la Baraza wakati wa zoezi la uelimishaji liliofanyika hivi karibuni katika eneo la hospitali ya KCMC. Picha na Mpigapicha Wetu

Wailalamikia TANESCO kutofuata ratiba mgao wa umeme

Na Zamda Mabada, Kilimanjaro

Wakazi wa Manispaa ya Moshi na vitongoji vyake wamelalamikia tatizo la kukatika kwa umeme kusikokuwa na ratiba maalumu na kudai kuwa kitendo hicho kinachangia kwa kiasi kikubwa kuzorota kwa biashara na uchumi wa wakazi wa mji huo.

Wakiongea kwa nyakati tofauti wakati wa programu za uelimishaji kwa makundi mbalimbali ya watumiaji wa huduma za nishati na maji mjini Moshi zinazotekelawa na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), wakazi hao walieleza kusikitishwa kwa na kitendo cha kukatikatika kwa umeme na pia ratiba ya mgao wa umeme kutofuatwa hivyo kuathiri shughuli za kiuchumi katika mji wa Moshi.

"Sisi wananchi tunakubaliana na hali ya umeme kukatika kutoke na upungufu wa uzalishaji lakini cha kusikitisha ni kuwa, hata ule kidogo ambao tunatakiwa kuupata hatuupati ipasavyo. Tunaiomba TANESCO itoe taarifa kama kuna katizo la umeme ili wafanyabiashara wanaotegemea nishati hiyo wajiandae kukabiliana na

changamoto hiyo," alisema ndugu Abdul Swai mkazi wa Bomambazi.

Naye ndugu Boniventure Joseph, mkazi wa KCMC, alieleza kuwa nishati ya umeme ni muhimu katika shughuli za kijamii na kiuchumi, hivyo Shirika luhakikishe linafuata ratiba liliyojiweka ili kuwawezesha wananchi kufanya shughuli za uzalishaji kwa ufanisi kulilingana na ratiba hiyo huku akionesha kuwa baadhi ya maeneo yanathirika zaidi kuliko mengine.

"Nawasihi TANESCO waifanyie kazi changamoto hii ili kuweka usawa kwa watumiaji wote pia kuondoa dhana kuwa kuna maeneo ni muhimu na mengine sio muhimu," alieleza ndugu Boniventure.

Boniventure aliiomba TANESCO kuboresha utoaji huduma ya umeme na taarifa kwa wateja wake ili kuhakikisha taarifa zote zinazohusiana na katizo la huduma ya umeme zinawafikia wakazi wa maeneo hayo kwa wakati.

"Niwaombe tu TANESCO kuhakikisha wanatimiza wajibu wao wa kutoa taarifa za katizo la umeme na ratiba iliyowekwa ifuatwe. Pia ifahamike kuwa mteja wa umeme kupata taarifa ni moja ya haki za msingi za mtumiaji wa huduma," aliongeza ndugu Boniventure.

Kwa upande wake, Afisa Uhushiano wa TANESCO Mkoa wa Kilimanjaro Bi. Mwanaisha Mbita alikiri kuwa ndani ya mji wa Moshi kwa sasa kuna mgao wa umeme unaotokana na upungufu wa uzalishaji kwenye vyanzo vya umeme na hii imepelekea changamoto ya kukosekana kwa umeme zaidi ya ratiba ya kawaida.

Bi. Mbita pia alieleza kuwa chanjamoto ya kukatika kwa umeme ndani ya mji wa Moshi imekuwa ikisababishwa na sababu zingine mbalimbali za kiufundi na inapotokea hali hiyo, Shirika limekuwa likifanya jitihada za makusudi kuhakikisha huduma inarejea haraka.

"Changamoto hii ya kiufundi imekuwa ikisababishwa na mfumo wa uzalishaji umeme kuzidiwa na kuperlekea baadhi ya njia za umeme zisizokuwa kwenye ratiba tuzizime ili kunusuru mfumo mzima usipate matatizo. Hata hivyo kukatika huku nje ya ratiba huwa hakuzidi masaa matano kwa eneo husika," alisema Afisa Uhushiano huyo wa TANESCO.

Alitaja sababu nyingine ni kutoke kwa hitilafu kwenye miundombinu ya umeme hivyo kulazimika kuzima umeme ili kutatua changamoto iliyojitokeza kwa wakati huo na kwamba hali inapotengamaa kwenye vituo huduma ya umeme hurejeshwa haraka.

Alimalizia kwa kueleza kuwa taarifa ya ratiba ya mgao wa umeme kwa mkoa wa Kilimanjaro hutolewa kwa njia kuu tatu ambazo mitandao ya kijamii kama vile WhatsApp, matangazo kwenye redio hasa kituo cha Banana FM na kupeleka barua kwenye taasisi na nyumba za ibada **Inaendelea Uk. 38**

Washauriwa kuboresha ubora wa maji Biharamulo

Na Anadorice Komba, Kagera

Wananchi wa mitaa mbalimbali katika Halmashauri ya Mji wa Biharamulo, wameishauri Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Biharamulo (BUWSA) kutatua kero ya muda mrefu ya mabomba kutoa maji machafu na yasiyo salama.

Ushauri huo umetolewa hivi karibuni na wakazi hao wakati wa kuchangia mada kwenye mkutano wa taftishi ulioandaliwa na Mamlaka ya Udhhibit wa Huduma za Nishati (EWURA) na kufanyika kwenye miji wa Biharamulo.

Watumiaji hao walibainisha adha kubwa wanayoipitia ya kupata maji machafu ambapo imekuwa ikiwalazimu kutafuta au kununua majisafi ambayo ni ghali kutoka vyanzo vingine ili kuepuka madhara ya kiafya kutokana na aina ya maji wanayopata toka BUWSA.

Akiongea kwenye mkutano huo Bi. Janeth Maximilian mkazi wa Majengo "B" ambaye ni mmoja wa waathirika waliowahi kupata maji machafu katika eneo lake hasa nyakati za mvua alisema kuwa wanashukuru mtaa wa Majengo maji wanapata maji lakini ni machafu na hivyo wanaingia gharama tena za kununua maji ya kunywa na kufulia nguo hasa nyeupe.

Naye Bw. Musozi Issa mkazi wa Mtaa wa Maendeleo alisema kuwa, kipindi cha mvua maji yanayotoka katika mabomba ni machafu na huwa hawayatumii badala yake wanakinga maji ya mvua kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

"Kinachosikitisha ni kwamba maji tunapata ila ni machafu kiasi kwamba hatuyatumii na badala yake tunaishia kuyamwaga lakini mwisho wa mwezi tunaletewa ankaru ya matumizi ya maji. Hali hii inatumiza sana na kama BUWSA inataka kuongeza bei basi tunam-

womba Mkurugenzi atuhakikishie wateja wake kuwa tutapata majisafi na salama," alisema Bwana Musozi.

Bi. Betida Fidelis mkazi wa mtaa wa KKKT hakusita kutoa kero yake na alinukuliwa akisema, "mimi ni mfanyakishara wa nyumba ya kulala wageni na ninajikuta siwezi kufua mashuka meupe kwa katumia maji ya BUWSA, hali hii inanifanya nitumie gharama nyingine ili kununua maji ya kufulia na ya kuoga kwa wateja."

Akitolea ufanuzi juu ya kero hiyo, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Biharamulo (BUWSA) Mhandisi Suraj Abdul alikiri kuwepo kwa changamoto hiyo kwa muda mrefu sasa.

"Ni kweli kumekuwa na changamoto ya maji machafu katika eneo tunalolihudumia ambapo wakati mwingine maji yanakuwa na rangi, hali hii hutokana na mvua zinaponyesha kwenye maeneo ya vyanzo vyetu vya maji na hivyo maji kuchafuka," alisema Mhandisi Abdul.

Alisema kwamba hali hii itakwisha pale watakopata bei mpya kwa sababu moja ya jambo ambalo wanaliahidi kufanya ni pamoja na kununua vifaa ambavyo vitasaidia kuchunguza ubora wa maji, kwani kwa hivi sasa wanalazimika kusafiri hadi Bukoba Manispaa kwenda kupima ubora wa maji.

"Endapo bei mpya tunazoomba zitaidhinishwa tutaweza kununua dawa za kutosha ili kutibu maji, sambamba na hilo tuna mradi wa kujenga chujio la maji katika eneo la Ruziba amba unaendelea na umefikia hatua nzuri ambapo maji yatachujwa kuondoa uchafu wote," alieleza Mhadisi Abdul.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Kagera (RCC), Najim Bwanika alisema moja ya haki ya mtumiaji wa huduma za maji ni usalama katika huduma anazozitumia, zisiwe zinazohatarisha maisha yake.

"Tunatoa wito wetu kwa BUWSA kuhakikisha ubora wa maji unazingatiwa katika nyakati zote kwa kusafisha matanki ya kuhifadhi maji mara kwa mara na kuharakisha ujenzi wa machujio yenye ubora ili kuondoa changamoto hiyo," alisema Bwanika.



Mmoja wa watumiaji wa huduma za maji mjini Biharamulo (aliyesimama kushoto) akitoa maoni yake wakati wa mkutano wa taftishi uliofanyika mwezi Agosti 2023 mjini Biharamulo kwa ajili ya kujadili ombi la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Biharamulo (BUWSA) la kutaka kubadilisha bei za maji. Picha na Anadorice Komba

Fahamu taratibu za kuomba leseni za umeme na aina zake

Na Catherine Charles, Ilala

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ndiyo inayosimamia uzalishaji na usambazaji wa umeme nchini. Mamlaka hii imepewa nguvu kisheria kuhakikisha taasisi au kampuni zote zinazojishughulisha na biashara za umeme zinifuata taratibu zilizowekwa.

Moja ya taratibu hizo ni kuwa na leseni za kuendesha shughuli zote zinazojihusisha na mambo ya umeme ikiwa ni kuzalisha umeme, kusambaza au kujenga miundombinu ya umeme kwenye majengo.

Ikiwa ni moja ya jukumu la Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kutoa elimu kwa watumiaji wa huduma hizo zinazodhibitwa na EWURA, makala hii inalenga kubainisha utaratibu wa kufuata kwa yejote anayehitaji leseni za ufungaji wa mifumo ya umeme na aina za leseni zitolewazo.

Sheria ya Umeme Sura ya 131, na Kanuni ya 4(1) ya Kanuni za Umeme Huduma za Ufungaji Mifumo ya Umeme za mwaka 2022, zilizochapishwa na Gazeti la Serikali Na. 113 inaelezea kuwa mtu yejote hata-

ruhusiwa kufanya shughuli za kufunga mifumo ya umeme bila kuomba na kupata leseni inayotolewa na EWURA.

Kifungu cha 5 cha Sheria ya Umeme Sura ya 131 inaelezea utaratibu wa uombaji wa leseni kwa watu wanaotaka kujishughulisha na kazi pamoja na shughuli za umeme kama ifuatavyo;

■ Mwombaji atatakiwa kuwasilisha maombi ya leseni ya kufunga mifumo ya umeme kuitia fomu na kwa namna ilivyoanishwa katika tovuti ya EWURA.

■ Maombi hayo ya leseni yatatakiwa kuambatana na:-

- Nakala za vyeti vya elimu ya mwombaji vilivyothibitishwa.
- Wasifu wa mwombaji leseni.
- Picha ya pasipoti ya rangi iliyopigwa kipindi cha karibuni.
- Kibali cha kufanya kazi kwa mwombaji ambaye siyo raia wa Tanzania.
- Mwombaji atawajibika kulipa ada ya maombi isiyorudishwa.
- Mwombaji awe na kitambulisho halali cha mlipa kodi.

■ Kifungu cha 6 cha Sheria ya Umeme Sura ya 131 kinalezea aina za leseni za ufungaji wa mifumo ya umeme na yafuatayo ni madaraja ya

leseni zinazotolewa na EWURA;-

a) Daraja "A": Daraja hili hutolewa kwa ajili ya kufanya kazi za ufungaji mifumo ya umeme katika msongo wa umeme wa aina zote.

b) Daraja "B": Daraja hili hutolewa kwa ajili ya ufungaji mifumo ya umeme katika msongo wa katika mpaka kiasi cha msongo wa volti 33,000.

c) Daraja "C": Daraja hili hutolewa kwa ajili ya ufungaji mifumo ya umeme katika msongo wa umeme usiozidi volti 1,000.

d) Daraja "D": Daraja hili hutolewa kwa ajili ya ufungaji mifumo ya umeme usiozidi volti 230.

e) Daraja la "W": Daraja hili hutolewa kwa ajili ya ufungaji mifumo ya umeme chini ya usimamizi wa mwenye leseni Daraja A, B, C, D, S1, S2, S3 au D.

f) Daraja la "S1": Daraja hili hutolewa kwa ajili ya ufungaji mifumo ya umeme katika msongo wa aina zote.

g) Daraja la "S2": Daraja hili hutolewa kwa ajili ya kufanya kazi maalum za ufungaji mifumo ya umeme mpaka msongo wa volti 33,000

h) Daraja la "S3": Daraja hili hutolewa kwa ajili ya kufanya kazi maalum za ufungaji mifumo ya umeme mpaka msongo wa volti 1,000.

Bila kujali mipaka ya kazi iliyoainishwa, mtu anayemiliki leseni A, B, C na D hataruhusiwa kufanya kazi yoyote iliyo chini ya leseni maalum pasipo kuwa na leseni husika.

Makala

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
MOSHI (MUWSA)

FAHAMU SHERIA ZA MAJI

Kwa mujibu wa Sheria **Na. 5** ya usambazaji maji na usafi wa mazingira ya mwaka 2019, kifungu **Na. 61-69** kinakataza kufanya uharibifu au kuingilia miundombinu ya Majisafi na Majitaka. Mtu yejote atakaekutwa na kosa hilo faini yake ni Tsh. **500,000** hadi **50,000,000**, kifungo kisichopungua mwaka 1 hadi miaka 5 au vyote kwa pamoja na kulipa gharama zote za uharibifu huo.

HUDUMA KWA MTEJA | SIMU YA BURE **0800110074**

muwsa moshi_muwsa Mamlaka ya majisafi Moshi Majimoshi

PIGA *152*00#

MAJI KIGANJANI

Huduma Za Serikali

- 1. Malipo
- 2. Afya
- 3. Uliza, Utambuli
- 4. Nishati, Madini, Usafiri
- 5. TRA
- 6. Maji
- 7. Kilimo, Ufugaji
- 8. Mafalabu
- 9. Matalamiko, Sheria na Haki

** Cancel

Huduma za Maji za Pamoja

- 1. Ombi la Maji
- 2. Kurudishwa Maji
- 3. Uliza Deni lako
- 4. Uliza Taarifa za Malipo
- 5. Tokeni zako
- 6. Uliza Bili

@muwasamusoma +255 800 110 108

Umuhimu wa kutunza miundombinu ya umeme

Na Josephine Ntaumenya, Mwanza

Miundombinu ya umeme ni sehemu muhimu sana ya maendeleo ya nchi, ikiwa ni msingi wa uchumi wa viwanda, huduma za afya, elimu na maendeleo ya kiteknolojia.

Makala hii inaangazia umuhimu wa kutunza miundombinu ya umeme nchini Tanzania na jinsi inavyoweza kuathiri maendeleo na ustawi wa nchi pale inapokuwa imeharibiwa.

Baadhi ya mifano ya miundombinu ya umeme ambayo isipotunzwa na kulindwa hupelekea madhara makubwa kwenye utoaji wa huduma ya umeme ni pamoja na nguzo za umeme, nyaya za umeme, mita, transfoma, mabwawa ya kuzalishia umeme, mito na vituo vya uzalishaji na usambazaji wa umeme.

Miundombinu hii yote hujengwa/hununuliwa kwa gharama kubwa ndio maana mara nyingi hujengwa kwa awamu. Miundombinu hii

“
Kutunza miundombinu ya umeme husaidia kupunguza upotevu wa nishati hii. Kwa mfano miundombinu ya usambazaji wa umeme isiyovuja inamaanisha kwamba umeme unaweza kufika kwa watumiaji bila kupotea njiani na hivyo kuongeza ufanisi wa matumizi ya nishati hiyo.

isipolindwa na ikaachwa kuharibiwa hufifisha maendeleo ya nchi kwani Serikali hujikuta badala ya kuongeza miundombinu mipyä huendelea kufanya ukarabati mindombinu ileile kila mwaka. Jukumu la kuitunza miundombinu hii ni la kila mwananchi wa Tanzania na pia ni kitendo kinachoonesha uzalendo.

Kwenye makala hii Mhandisi wa Afya na Usalama kutoka TANESCO kanda ya Ziwa Julius Venance aneleza umuhimu na faida za kutunza miundombinu ya umeme kwa manufaa ya wananchi na maendeleo ya taifa. Mionganoni mwa faida za kutunza miundombinu ya umeme ni kama ifuatavyo:-

Upatikanaji wa huduma ya uhakika:

Mhandisi Venance anaeleza kuwa miundombinu ya umeme ikitunzwa husaidia kuboresha upatikanaji wa huduma ya umeme kwa ufanisi zaidi. Huduma ya umeme ni muhimu kwa watumiaji na kunapokuwa na



MARA

Tupigie Namba: 0748 550 000  0758 346 869



KWA MSAADA ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA VIONGOZI WETU KWA NAMBA ZIFUATAZO

Afisa Mahusiano huduma Kwa Wateja Mkao wa Mara	0735 885 580
Meneja wa Mkao wa Mara	0735 000 335
Meneja wa Wilaya ya Ronya	0767 973 435
Meneja wa Wilaya ya Tarime	0736 792 525
Meneja wa Wilaya ya Bunda	0736 173 648
Meneja wa Wilaya ya Serengeti	0763 083 265
Meneja wa Wilaya ya Butiama	0715 397 797
Mhandisi wa Matengenezo	0767 534 741

Tanesco Tunayaangaza Maisha yako!

“**Tanesco Niudumie**”
 “**Tanesco Niabarishe**”
 “**Tanesco Tupime**”

changamoto kutokana na miundombinu iliyopitwa na wakati au inayokabiliwa na matatizo inaweza kusababisha kusuasua katika utoaji wa huduma hiyo. Hujuma au uharibifu wa miundombinu unaweza kuathiri usambazaji na upatikanaji wa huduma ya umeme, na hivyo kuathiri watumiaji na uchumi wa watu binafsi na taifa kwa ujumla.

Kukuza uchumi na upatikanaji wa ajira

Miundombinu ya umeme ikiwa bora husaidia katika hatua za kukuza uchumi wa nchi. Viwanda huhitaji umeme wa kuaminika kwa ajili ya uzalishaji lakini pia biashara ndogo na za kati nazo huhitaji umeme, hivyo basi panapokwuwe na umeme wa uhakika uwekezaji wa viwanda na biashara huongezeka na hivyo kuchochea upatikanaji wa ajira kwa watananza.

Kupunguza upotevu wa umeme kuitia miundombinu bora ya umeme

Kutunza miundombinu ya umeme husaidia kupunguza upotevu wa nishati hii. Kwa mfano miundombinu ya usambazaji wa umeme isiyovuja inamaanisha kwamba umeme unaweza kufika kwa watumiaji bila kupotea njiani na hivyo kuongeza ufanisi wa matumizi ya nishati hiyo. Kupunguza upotevu wa nishati hiyo pia husaidia watu wengi zaidi wapate huduma hiyo kwa kuwa mahitaji ya wateja wengi zaidi wanaweza kufikiwa.

Huboresha upatikanaji na utoaji wa huduma bora za afya na elimu

Sekta za afya na elimu zinategemea upatikanaji wa umeme wa kuaminika ili kutoa huduma bora. Hospitali na vituo vya afya iwe ni vya umma au binafsi hutumia umeme kwa vifaa vya matibabu na uendeshaji wa maabara. Shule nazo hutumia umeme kama chanzo cha mwanga, kuunganisha vifaa vya kujifunzia kama vile kompyuta, matumizi ya maabara

n.k. Ni dhahiri kwamba bila huduma ya umeme za uhakika katika vituo vya afya au shule na vyuo hakuwezi kuwa na ufanisi wa huduma hizo.

Kuvutia uwekezaji wa kigeni

Uwekezaji wa kigeni unaweza kuleta fursa za maendeleo na teknolojia mpya nchini Tanzania. Miundombinu ya umeme inayofanya kazi vizuri ni jambo linalovutia wawekezaji wa kigeni.

Wawekezaji wanahitaji umeme wa uhakika na nafuu kwa shughuli zao. Kwa mfano, ujenzi wa kituo cha kufua umeme kwa gesi asilia cha Kinyerezi I & II unaweza kuwa mfano wa jinsi Tanzania inavyoendelea kuwawutia wawekezaji wa kigeni katika suala zima la miundombinu ya umeme yenye kuzalisha umeme wa uhakika.

Kwa hiyo, kwa kuendelea kutunza na kulinda miundombinu ya umeme, Tanzania inaweza kuendelea kufikia malengo ya maendeleo na ustawi wa wananchi wake. Hili ni jukumu la kila mwananchi mmoja mmoja kuwa na uchungu na kuthamini jitihada za Serikali na TANESCO katika kutoa huduma ya umeme. Hii inaenda sambamba na kuendelea kujielimisha na kufichua wale wote wenye nia ovu ya kuihujumu TANESCO.

“

**Kwa kuendelea
kutunza na kulinda
miundombinu ya
umeme**, Tanzania
inaweza kuendelea
kufikia malengo ya
maendeleo na ustawi
wa wananchi wake.
Hili ni jukumu la kila
mwananchi mmoja
mmoja kuwa na
uchungu na kuthamini
jitihada za Serikali
na TANESCO katika
kutoa huduma ya
umeme. Hii inaenda
sambamba na
kuendelea kujielimisha
na kufichua wale wote
wenye nia ovu ya
kuihujumu TANESCO.

KAGERA
SASA TUMEKUFIKIA

HUDUMA KWA WATEJA

Sasa unaweza kuwasiliana nasi kwa namba **0748550000** muda wowote kwa huduma bora na za uhakika

NIHUDUMIE NAMBA
0748550000

1 2 3
4 5 6
7 8 9
*, 0, #

#TupoKazini

Facebook Twitter Instagram YouTube

Huu hapa utaratibu wa kukarabati miundombinu ya maji

Na Brenda Magoma, Iringa

Wakazi wa Manispaa ya Iringa na vitongoji vyake wamehoji kuhusu utaratibu unaopaswa kutumika katika kukarabati miundombinu ya bomba linalopeleka maji kwa mteja ili kubaini jukumu hilo ni la nani pamoja na utaratibu unaopaswa kutumika pindi uharibifu unapotokea.

Wakiongea kwa nyakati tofauti walipotembelea banda la EWURA CCC-Iringa wakati wa maonesho ya utalii ya "Karibu Kusini Septemba 2023," wakazi hao walawasilisha hoja na malalamiko yao amba-po kati ya malalamiko 10 yalipokelewa, 6 kati ya hayo yalihusu mivujo ya maji na bili kubwa.

Kupitia malalamiko hayo EWURA CCC ilibaini kuwa changamoto za bili kubwa zilizotajwa na wateja hao kwa kiasi kikubwa zilikuwa zimesababishwa na mivujo ya maji mbele za mita huku baadhi yao wakiwa hawajui ni nani mwenye jukumu la kukarabati miundombinu ya maji pindi ikituwa baada ya mita jambo ambalo limekuwa likisababisha hasara

“Kanuni zimebainisha wazi wahusika wanaopaswa kufanya matengenezo na utaratibu wa kuchukuliwa katika kutekeleza ukarabati huo. Aidha makala imebainisha maeneo yanayopaswa kukarabatiwa na mto huduma au mteja

na bili kubwa kwa wateja.

Kupitia makala hii mwandishi anaelezea nani mwenye jukumu la kukarabati mabomba ya maji yanapeleka huduma kwa wateja (service line) na nani mwenye jukumu la kukarabati miundombinu ya maji iliyopo mbele ya mita ya mteja. Hapa watumiaji watajifunza na kuona wajibu wao upo wapi

katika kukarabati miundombinu ya maji hivyo kupunguza hasara za bili kubwa na uvujaji wa maji.

Kupitia Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira (Ubora wa Huduma na Leseni) za Mwaka 2020; Tangazo la Serikali Na.849. Kanuni zimebainisha wazi wahusika wanaopaswa kufanya matengenezo na utaratibu wa kuchukuliwa katika kutekeleza ukarabati huo. Aidha makala imebainisha maeneo yanayopaswa kukarabatiwa na mto huduma au mteja.

Kanuni ya 38 ya Kanuni tajwa hapo juu inaweka wazi kuwa bomba linalopeleka maji kwa mteja (service line) linabaki kuwa mali ya mteja lakini chini ya uangalizi wa mto huduma na litakarabatiwa na mto huduma kwa gharama zake; isipokuwa kama mteja ameomba mwenyewe kuhamishwa kwa bomba hilo au kama uharibifu umefanywa na mteja mwenyewe, Kanuni ya 39(1) (a&c).

Kuhusu matengenezo, Kanuni ya 39(1)(b) ya Kanuni tajwa inaelekeza kuwa mto huduma atawajibika kukarabati "service line" kabla ya mita na mteja atasimamia miundombinu yake baada ya mita na kuwajibika kukarabati/kurekebisha mivujo yoyote itakayo jitokeza.

Kanuni ya 39(1)(e) inaelekeza kuwa mto huduma atawajibika kutunza usalama wa dira (mita) ya kupimia maji aliyoifunga kwa mteja. Wajibu wa mteja kwene suala hili ni kutoa taarifa kwa mto huduma juu ya uharibifu wowote unaowenza kujitokeza, Kanuni ya 39(2)(a&b).

Hatua muhimu za kuchukua endapo mtumiaji utagundua kuna uvujaji wa maji baada ya mita:

Funga koki (gate valve) ya maji iliyonyuma ya mita yako ili kuzuia upotevu wa maji usiendelee amba-o ungesababisha kupata bili kubwa.

Muite fundi ili aweze kuangalia na kubaini sehemu inayouju na kufanya marekebisho kwa haraka.

EWURA CCC inawashauri watumiaji wa huduma za maji kuchunguza miundombinu ya maji mara kwa mara na kutokupuzia mvujo mdogo. Pia inashauriwa watumiaji kuwa na utaratibu wa kukagua miundombinu ya maji katika majengo yao ili kujiridhisha kuwa hakuna maji yanayopotea.



**WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI
WA MAZINGIRA IRINGA (IRUWASA)**

“Epuka kusitishiwa huduma ya maji. Lipa bili yako leo uendelee kufurahia huduma za IRUWASA.”

LIPA SASA

m-pesa tigo pesa airtel money halopesa NMB CRB BANK

Wasiliana Nasi Bure

0800 110 122 @iruwa.sa @Iruwasa_Iringa

Afidiwa kutokana na hitilafu ya umeme

Na Noela Ntiluvakule, Pwani

Mkazi mmoja wa Kata ya Pangani Wilayani Kibaha ndugu Mariam Mahala amelipwa fidia ya kiasi cha fedha za kitanzania shilingi laki sita (600,000/-) baada ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kuliagiza Shirika la Umeme, Tanzania (TANESCO) kumlipa kiasi hicho cha fedha mteja wake huyo ku-fuatia kuunguliwa na mali zake kulikotokana na hitilafu ya umeme.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya kikao cha usuluhishi kilichofanyika tarehe 18.09.2023 mjini Kibaha ambapo katika kikao hicho pande zote mbili zilikubaliana chini ya Uenyekiti wa EWURA kwamba TANESCO imlipe Bi. Mariam fidia ya nusu ya thamani

Niliwaandikia barua ya malalamiko
ya kudai kufidiwa vifaa vyangu, lakini sikuridhishwa na majibu yao hatimaye nikaenda EWURA CCC ili kupata msaada zaidi

ya gharama ya vitu vyake ambayo vilungua kwa kuzingatia uchakavu wa baadhi ya vifaa hivyo.

Akitoa ufanuzi kuhusu tukio hilo Bi. Maariam alisema tarehe

21.04.2023 katika eneo la Pangani kulitokea hitilafu ya umeme ambayo chanzo kikiwa ni kugusana kwa nyaya zinazopeleka umeme katika kiwanda cha "Food Industry Production" na zile zinazopeleka umeme kwene makazi ya watu na hivyo kupelekeea kuungua kwa mita za umeme na vifaa vya majumbani katika nyumba za wakazi wa eneo hilo.

"Cha kushangaza baada ya tukio hilo tuliona TANESCO wakichukua hatua moja tu ya kubadilisha mita zao zilizoungua na kuweka mita mpya lakini sisi wananchi walituacha pasipo kutufidia vifaa vyetu vilivyoungua," alieleza Bi. Mariam.

Alieleza kuwa, kutokana na TANESCO kutoonesha hali ya kuwajali wateja wake, ye ye aliamua kuandika barua ya malalamiko dhidi ya TANESCO akidai kulipwa fidia ya vifaa vyake.

"Niliwaandikia barua ya malalamiko ya kudai kufidiwa vifaa vyangu, lakini sikuridhishwa na majibu yao hatimaye nikaenda EWURA CCC ili kupata msaada zaidi," alisema Bi. Mariam.

Aliishukuru EWURA CCC Mkao wa Pwani kwa kumsaidia kupata haki yake, ambayo pasipo msaada huo pengine haki yake ingepotea.

Pia aliomba EWURA CCC izidi kutoa elimu zaidi kwa umma kwani wapo watu wengine hupatwa na madharahayos lakini hawajui pa kwenda na kuishia kupoteza haki zao.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkao wa Pwani ndugu Saidi Kabirigi alimpungeza Bi. Mariam kwa kuwa na ujasiri wa kudai haki yake dhidi ya TANESCO.

"Nilitembelea eneo ambalo watumiaji wa umeme walathirika kwa kuunguliwa samani zao na kubaini kuwa waathirika walikuwa wengi lakini aliye thubutu kudai fidia ni mmoja tu," alisema Kabirigi, huku akiongeza kuwa ni muhimu watumiaji kudai haki zao wanapopata changamoto kwani haki siku zote hudaiwa.

Kabiringi alisema Kamati yake inalo jukumu la kuwaelimisha wananchi ili kutambua haki zao za msingi na wajibu wao kuhusu huduma za nishati na maji. Kwa kufanya hivyo itazidi kuwajengea uelewa watumiaji hao kuhusu huduma husika na pia kuwapa changamoto watoa huduma ili kuboresha huduma zao.

Uwajijibikaji

ZOEZI LA UBADILISHAJI MITA ZINAZOANZA NA 04 NA 05
PIGA SIMU 0748550000 KUTOA TAARIFA YA MITA YAKO

#TupoKazini

Fahamu muda wa ukomo wa malalamiko ya huduma ya maji

Na Ramadhan Kakende, Rukwa

Hapana shaka kuwa malalamiko katika huduma yoyote huchochea ufanisi na ubora wa huduma toka kwa mto huduma. Kwa upande mwininge, ushughulikiaji wa malalamiko ya wateja katika muda husika huleta hali ya kuridhika kwa mteja na pia hutengeneza mazingira mazuri ya mahusiano kati ya mto huduma na mtumiaji.

Hali si tofauti katika huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA). Kama huduma inayohuishwa mto huduma na mtumiaji wa huduma hakuna shaka kuwa malalamiko hayawesi kuko-sekana baina ya pande hizi mbili na hasa kwa mtumiaji.

Kifungu cha 34 cha Sheria ya EWURA kinamtaka mto huduma kushughulikia malalamiko dhidi yake kwa suala lolote linalohusu us-

ambazaji, uwezekano wa kusambaza huduma au mapendekezo ya usambazaji wa huduma.

Ikumbukwe kuwa mtu yejote akiwa mtumiaji wa huduma zinazodhibitiwana EWURA anayo haki ya kulalamika kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Mamlaka inatakiwa kikanuni na kisheria kushughulikia malalamiko hayo.

Baraza la ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) linayo mamlaka kisheria ya kulalamika kwa niaba ya watumiaji au mwakilishi aliyeidhinishwa na upande unaolalamika. Aidha kikundi cha watu pia kinaweza kuwasilisha malalamiko kwa kuambatanisha nyaraka zinazotakiwa.

Huduma bora ya majisafi na usafi wa mazingira ni muhimu sana katika ustawi wa maisha ya mwanadamu, hivyo basi mamlaka za maji zinatakiwa kuhakikisha mtumiaji anapata huduma ya maji iliyo bora na nafuu kwake.

Kwa kuzingatia hili EWURA imeweka utaratibu wa utatuvi wa malalamiko ya watumiaji wa huduma za maji Pamoja na ukomo wa muda wa kuwasilisha malalamiko hayo ili kutengeneza ubora wa huduma pamoja na ustawi wa watumiaji.

Ukomo wa muda hutegemea aina ya malalamiko na malalamiko yatakayowasilishwa baada ya ukomo wa muda hayatafanyiwa kazi. Ni muhimu watumiaji kujua ukomo huu wa muda ili wasipoteze haki zao. Sababu ya kuweka ukomo wa muda ni kuwezesha Mamlaka kufanya kazi kwa wakati na kukusanya ushahidi ambaa utasaidia katika kutatua suala hilo kwa uadilifu.

Makala hii inachambua makundi ya malalamiko na kipindi kili-chowekwa kwa mujibu wa Kanuni za EWURA za Utaratibu wa Utatuvi wa malalamiko za Mwaka 2020 (26) (1) jedwali namba (4) ili kuwezesha upatikanaji wa haki kwa pande zote za mlalamikaji na mlalamikiwa.

a) Kukatishwa kwa huduma ya maji kinyume cha sheria: Muda uliowekwa ni kipindi cha miezi kumi na mbili tu.

Kukatishwa huduma kinyume cha sheria maana yake ni kukatiwa maji pasipo kuzingatia kanuni na utarat-

Rudisha Huduma ya Maji bila kulipa Faini!

Wiki ya Huduma kwa Wateja TUKIO LA UKATAJI KEKI

KAZI IENDELEE

Katika Kuadhimisha Wiki ya Huduma Kwa Wateja MUWASA yakata keki na Wateja wake

Wasiliana Nasi

Tembelea Ukurasa wetu www.muwasa.go.tz

f **i** **t** **@muwasamusoma**

LIPIA
HUDDUMA YA MAJI

MTEJA WETU, NDIYO FAHARI YETU

NI RAHISI, TUMIA MENU YA MTANDAO UNAUTUMIA

*150*00#	*150*01#	*150*60#	*150*88#	*150*71#

UNAWEZA KULIPIA KWA WAKALA

CRB BANK **NMB** *The bank that lists*

- CHAGUA LIPA BILI
- MALIPO YA SERIKALI
- INGIZA NAMBA YA MALIPO Mfano: 99444*****
- INGIZA KIASI CHOTE UNACHODAIWA
- WEKA NAMBA YA SIRI Mfano: *****

bu. Kanuni ya 57 ya Kanuni za Ubona wa Huduma za maji na Usafi wa Mazingira za mwaka 2020 kifungu (3) inasema "Ukataji wa huduma usifanywe siku za ijumaa baada ya saa sita, jumapili na jumamsoi na siku za sikukuu. Endapo imetokea mtumiaji amekatiwa huduma katika siku hizo maana yake muda wa kuwasilisha lalamiko hilo usizidi miezi kumi na mbili (12) tangu kutokea kwa tatizo hilo.

b) Kuletewa ankara na tathmini ya gharama ya maunganisho ya maji isiyo sahihi: Muda uliowekwa ni ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili tu.

Lalamiko hili linazungumzia kuletewa ankara ya maji ambayo haiendani na matumizi yako aidha kwa makadirio au msoma mita kutokosoma mita kwa mwezi husika au kuletewa gharama za maunganisho ambazo haziendani na uhalisia wako. Malalamiko yote haya endapo mtumiaji anaona ana haki muda wa kuwasilisha malalamiko haya si zaidi ya miezi kumi na mbili (12) kuanzia tukio lilipotoka. Kumbuka kuwa Kanuni ya 42 (1) kutoka katika Kanuni za Ubora wa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira za mwaka 2020 inasema "lazima mtoe huduma

asome mita kujua matumizi halisi ya mtumiaji."

c) Kushindwa au kukataa kuunganisha huduma: Muda uliowekwa wa kuwasilisha lalamiko ni ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili tu

Kushindwa au kukataa kuunganisha huduma ya maji ni pale ambapo mteja mpya amefuata taratibu zote za kuunganishiwa huduma ya maji ikiwemo kufanya malipo na mtoe huduma kumcheleweshea kumuunganisha huduma hiyo. Katika mazingira hayo mtumiaji huyo hana budi kuwasilisha lalamiko hilo ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili (12). Kanuni ya 54 (1)(b) ya Kanuni tajwa hapo juu inasema kuwa "mtoe huduma atamuunganishia mteja mpya ndani ya siku saba (7) baada ya malipo."

d) Ubora duni wa huduma ya maji: Kipindi cha kuwasilisha lalamiko kilichowekwa ni ndani ya miezi kumi na mbili tu.

Ubora duni wa maji ni pale mtumiaji anapopokea maji yasiyokidhi viwango vya ubora viliviyewe kwa, kama vile maji yenye matope au yenye dawa zilizopitiliza. Hapa mtumiaji anatakiwa kutunza ushahidi na kulalamika mapema zaidi japo muda kikomo ni miezi kumi na mbili

(12).

e) Uharibifu wa vitu ikiwa ni matokeo ya matumizi ya huduma zinazodhibitiwa: Muda wa ukomo ni ndani ya miezi thelathini na sita tu.

Uharibifu huu ni ule unaotokana na huduma ya maji inayodhibitiwa hasa pale huduma hiyo inapoleta madhara aidha kwa mtumiaji mwenyewe au katika vifaa au mali zake. Ukomo wa kuwasilisha aina hii ya lalamiko ni miezi thelathini na sita tu (36).

Malalamiko katika huduma ya majisafi na usafi wa mazingira yanaweza pia kuhusisha lugha mbou kwa wateja, kutojibowi lalamiko kwa wakati na mengineyo. EWURA imeainisha baadhi tu ya malalamiko na kutoa muongozo wa ukomo wa muda wa kuwasilishwa kwake. Ifahaminke kuwa kuna baadhi ya malalamiko hayahitaji muda mrefu wa kusubiri kuyawasilisha kama ya kudai fidia kutokana na hitilafu ya huduma kwa lengo la kutopoteza ushahidi.

EWURA CCC inawasisitiza watumiaji wa huduma ya maji inayodhibitiwa na EWURA kuzingatia ukomo wa muda wa kulalamika na taratibu za ulalamikaji wake ili kue-puka kupoteza haki zao.

**MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA GEITA.
GEUWASA**

UTEKELEZAJI WA UJENZI WA MRADI WA UTANUZI WA MTAMBO WA KUTIBU MAJI NYANKANGA.

Ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya Majisafi kwa Wakazi wa Geita Mjini Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita inatekeleza ujenzi wa utanuzi wa mtambo wa kutibu maji eneo la Nyankanga, kukamilika kwa Mradi huu kutaenda kuongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka lita milioni 4 kwa sasa mpaka lita milioni 7 kwa siku.

Wasiliana Nasi Bure 0800 750 060

OPARESHENI KATA MAJI INAENDELEA WAHI LEO, LIPA BILI YAKO

LIPIA KWA NJIA YA SIMU

Ndugu mteja ulipaji wa bili za maji kwa wakati ni chachu ya maendeleo ili kuwafikishia huduma wateja wengine wengi zaidi.

Lipa bili yako mapema epuka usumbufu wa kukosa huduma.

WAKALA
tigo pesa
airtel money
telcom
mtn
bnp
m-pesa

LIPIA KWA NJIA YA BENKI

Shamilia
Kuwa mawenzi bank
Shamilia
Banks
M-Pesa
Kuwa mawenzi bank
Shamilia
Banks
M-Pesa

MAKONDE PLATFOM WATER SUPPLY AND SANITATION

Je, mto huduma ana wajibu gani kwa mteja?

Na Noela Ntiluvakule, Pwani

Neno wajibu si geni masikioni mwa wengi. Neno hili laweza kumaanisha jambo linalomlazimu mtu kulitimiza; jambo ambalo mtu hana hiari nalo katika kulifanya. Kwamba, tunaweza kusema kuwa wajibu ni tendo au vitendo ambavyo mtu au taasisi inalazimika kufanya kwa mujibu wa sheria au taratibu zilizowekwa, hii ina maana kuwa sheria au taratibu zilizowekwa ndio msingi wa wajibu kwa anayepaswa kuutekeleza.

Watoa huduma zinazodhibitiwa na EWURA, yaani Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira, Shirika la Umememe Tanzania (TANESCO), vifito vya mafuta, pamoja na gesi asilia, wote kwa pamoja wana wajibu wa kuhalikisha wanatoa huduma zenyenye ubora kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa.

Makala hii itatumia rejea ya Mikkataba ya Huduma kwa Wateja wa TANESCO na DUWASA ambazo zinatoa wajibu kwa watoa huduma hao katika utekelezaji wa majukumu yao na kufikia viwango vya huduma kama zilivyoainishwa katika mikataba hiyo. Hapa chini ni baadhi ya wajibu uliotajwa katika nyaraka hizo:-

i. Kuwahudumia wateja kwa kuhalikisha kuwa wanapata huduma zilizo bora ndani ya muda uliopangwa tena kwa weledi wa hali ya juu na huduma ziwe zinazokidhi viwango vya ubora kwa mujibu wa mikataba yao.

ii. Kuwa waadilifu na wawazi katika kuwahudumia wateja wa huduma za maji na nishati kwa umahiri bila ya kufanya upendeleo, kupokea rushwa, zawadi au ushawishi wa kifedha au mitazamo binafsi ya kisiasa inayoweza pelekea kuingilia utekelezaji wa majukumu yao katika kutoa huduma kwa wateja.

iii. Kutoa habari na taarifa kamili na sahihi kuhusiana na huduma wanazozitoa pamoja na shughuli za uendeshaji kwa ujumla ambazo zitajumuisha taarifa kuhusu sera,

miongozo na kanuni mbalimbali zinazohusu sekta na huduma zinazodhibitiwa, mkataba wa huduma kwa wateja, makatizo ya huduma na utatuvi wa malalamiko pindi yanapotokea.

iv. Kuwafidia wateja pale wanaposababisha hasara kutokana na kupatiwa bidhaa zenyenye dosari au huduma mbovu au uharibifu wa mali za mteja baada ya kuwa imehakikisha kwamba tatizo hilo halikusababishwa na mtumiaji wa huduma husika.

v. Kushauriana na wateja kuhusiana na huduma wanazozitoa hasa katika maeneo yanayohitaji maboresho endelevu ya huduma kwa kukuza ubunifu na kujifunza kulinda na kutunza miundombinu ili kudumisha huduma na mahusiano mazuri na wateja wao.

vi. Kufanya uchunguzi kwa wakati juu ya malalamiko yanayowasilishwa na wateja na kutoa mrejesho baada ya kumalizika kwa uchunguzi. Kwa malalamiko yanayowasilishwa kwa njia ya maan-

dishi mto huduma ana wajibu wa kuyajibu kwa maandishi ndani ya muda uliowekwa kulingana na aina ya tatizo. Kama tatizo haliteweza kutatuliwa ndani ya muda uliowekwa mto huduma anawajibu wa kumfahamisha mteja wake na sio kukaakimya.

vii. Kushirikiana na wateja katika kutunza na kulinda miundombinu kwa lengo la kufanya huduma wanazozitoa ziwe endelevu, hasa pale mteja anapota taarifa juu ya wizi, uhujumu wa miundombinu, ukosefu wa huduma, mivujo, utiririkaji wa majitaka au kuanguka kwa nguzo za umeme. Mto huduma ana wajibu wa kufanya kazi taarifa hizo kwa haraka ili kujenga imani na hamasa kwa wateja katika kuendeleva mahusiano mazuri. Pia itawasaidia watumiaji wa huduma kuwa katika mazingira bora na salama kwenye makazi yao.

viii. Kuhakikisha kuwa Mikkataba wa Huduma kwa Mteja una-fahamika kwa wateja kwa uwazi na unatekelezwa kikamilifu. Mto huduma anatakiwa kumpatia mteja wake mkataba wa huduma kwa wateja katika hatua za awali mteja anapoomba kuunganishwa na huduma husika. Hii itamsaidia mteja kufahamu haki na wajibu wake na taarifa zinazojitosheleza kuhusu huduma zitolewazo na mto huduma.

ix. Kuwaelimisha watumiaji wa huduma husika juu ya huduma wanazozitoa kuititia vyombo mbalimbali vya habari kama vile radio, running au mitandao ya kijamii ili jamii iwe na ufahamu zaidi juu ya sera, miongozo na kanuni mbalimbali zinazohusu sekta na huduma zinazodhibitiwa. Pia elimu juu ya masuala ya bei, utatuvi wa migogoro na masuala ya kiusalama ni ya muhimu kuzingatiwa.

Watumiaji wa huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA wanakumbushwa kuwa wajibu wa mto huduma ndiyo unaotoa haki ya mtumiaji. Hata hivyo, haki huenda sambamba na wajibu, hivyo watumiaji wa huduma za nishati na maji wanahimizwa pia kutimiza wajibu wao ikiwemo kutoa ushirikiano kwa watoa huduma, kutunza miundombinu na kulipa bili zao kwa wakati.



Watumiaji wa huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA

wanakumbushwa kuwa wajibu wa mto huduma ndiyo unaotoa haki ya mtumiaji. Hata hivyo, haki huenda sambamba na wajibu, hivyo watumiaji wa huduma za nishati na maji wanahimizwa pia kutimiza wajibu wao ikiwemo kutoa ushirikiano kwa watoa huduma, kutunza miundombinu na kulipa bili zao kwa wakati.



Mha. David Ngula, Mwenyekiti wa EWURA CCC akifungua Mkutano wa Nne wa Wafanyakazi wa Baraza, uliofanyika wilayani Bagamoyo mkoani Pwani. Picha na Dennis Ndau

Fanyeni kazi kwa bidii - Ngula

Na Anadore Komba, Kagera

Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), Mhandisi David Ngula amewaasa wafanyakazi wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha malengo yaliyowekwa na Baraza yanatimia kwa mafanikio makubwa.

Mha. Ngula ameyasema hayo alipokuwa akifungua mkutano wa 4 wa mwaka wa watumishi wa Baraza uliofanyika tarehe 21 Agosti 2023, mjini Bagamoyo mkoani Pwani.

Ngula amesema "natambua wafanyakazi mnajitoa katika kutekeleza majukumu yenu na mafanya kazi kwa ufanisi mkubwa lakini lazima tuongeze bidii ili malengo ya Baraza yaweze kufikiwa. Ni matarajo ya Baraza kuwa mtahitimisha kikao hiki kwa maazimio yatakayopapa nguvu ya kwenda kufanya kazi kwa bidii na uadilifu," alisema Mhandisi Ngula.

Alisema kuwa, kazi kubwa wanayofanya wafanyakazi ni kujitoa na

kutafuta maarifa toka katika vyanzo mbalimbali ili kuhakikisha watumiaji wa huduma za nishati na maji wana-pata huduma kulingana na kanuni na miongozo iliyopo.

"Watumiaji wa huduma za nishati na maji katika mikoa mliyopo wanatutegemea sana kuwawakilisha kwenye masuala mbalimbali yanayohusu huduma zinazodhibitiwa na EWURA, kwa hiyo tunatakiwa kuwa wabunifu na wenye kujitoa wakati wote ili kuhakikisha watumiaji wanafikiwa na wanatapa elimu,"

Alisema kikao cha watumishi ni muhimu kwa mustakabali wa kazi na majukumu ya Baraza ambacho pamoja na kujadili masuala ya kazi, pia kutakuwepo na masuala ya kuwajengea uwezo kuhusu masuala mtambuka ambayo yote yana lengo la kuongeza ufanisi wa kiutendaji.

Naye Bw. Ramadhani Kakende, Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala wa EWURA CCC mikoa wa Rukwa, alimshukuru Mwenyekiti wa Baraza kwa ujumbe aliota kwa wafanyakazi na kuahidi kufanya kazi yote aliyoylekeza.

"Binafsi nimenufaika sana na maelekezo ya Mwenyekiti na nikito-

ka hapa nitakuwa na nguvu mpya na kufanya kazi kwa kujituma ili kuhakikisha malengo ya Baraza yanafikiwa. Kwa uzoefu tutakaobadilishana hapa utatusaidia sote kukabili changamoto katika vituo vyetu nya kazi kwa kuongeza wigo na kuaminika kwa Baraza mionganoni mwa wateja wetu," alisema Bw. Kakende.

Naye Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza, Bi. Stella Lupimo akimshukuru Mwenyekiti wa Baraza, huku akiaahidi kwa niaba ya wafanyakazi wenzake kuwa yeye na timu yake ya wafanyakazi watahakikisha malengo ambayo Baraza limeyaweka yatafikiwa kwa kila mfanyakazi kutimiza wajibu wake.

"Tumesikia maneno mazuri toka kwa Mwenyekiti wetu hivyo ni wajibu wetu sasa tunaporudi katika ofisi zetu kuhakikisha kila mmoja anafanya kazi kwa uadilifu, kujituma na kwa maarifa ili tuweze kufikia malengo ya Baraza," alisema Bi. Lupimo.

Bi. Lupimo alisema kikao hicho cha wafanyakazi kimekuwa chachu kwa kuongeza ufanisi kwa watendaji wa EWURA CCC kwani watumishi kutoka ofisi zote za mikoa hukutana na kubadilishana uzoefu pamoja na kupeana mbinu mpya za kuwafikia watumiaji wa huduma za nishati na maji kwa ukaribu zaidi na mwisho aliliomba Baraza kuendelea kuan-daa vikao hivi kwani vinaboresha utendaji wa watumishi na ni sehemu ya motisha kwa wafanyakazi.



Baadhi ya wakazi wa Mtaa wa Anglikana 'A' Manispaa ya Sumbawanga wakiwa na hati ya hukumu waliyoipata hivi karibuni kutoka EWURA baada na ushindi wa shauri lao dhidi ya TANESCO kutohana na kuunguliwa vifaa vyao iliyoababishwa na hitilafu ya umeme. Picha na Mpigapicha Wetu

Asante EWURA CCC

Na Mwandishi wetu, Rukwa

Baadhi ya watumiaji wa huduma ya umeme katika Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa, wameliishukuru Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoani Rukwa, kwa kuwasaidia kupatikana kwa haki yao ya fidia kutoka TANESCO kufuatia kuunguliwa vifaa vyao kulikosababishwa na hitilafu ya umeme.

Wakazi hao 14 wa Mtaa wa Anglikani "A" wameishukuru EWURA CCC baada ya tukio la ulipwaji fidia lilofanyika hivi karibuni baada ya wakazi hao kuwasilisha malalamiko yao kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na kushinda kesi hiyo.

EWURA iliamuru TANESCO kuwalipa kiasi cha zaidi ya shilingi Milioni 10 kama fidia baada ya kuthibitika kuwa wananchi hao waliumguliwa vifaa vyao mbalimbali vya umeme kutohana na hitilafu ya umeme iliyotheke mwanzoni mwa mwaka 2023.

Akizungumza kwa furaha baada ya kupokea malipo yake, Mwenyekiti wa Mtaa wa Anglikani "A" Bi. Adelina Mwanisenga ambaye alipokea kiasi cha shilingi 112,500, ikiwa ni fidia ya

“
**Kipekee naishukuru
EWURA CCC**

Sumbawanga kwa kusimama nasi wananchi wa mtaa wa Anglikani 'A' tangu mwanzo wa lalamiko mpaka mwisho na katuongoza kwa kutupatia elimu...

kuunguliwa vifaa vyake vya umeme (TV na Kisimbuzi) alieleza kuwa yeye na wenzake hao baada ya kupata changamoto hiyo walilikifisha lalamko lao mbele ya ofisi ya EWURA CCC ili kuwasaidiwa kudai fidia zao.

"Kipekee naishukuru ofisi ya EWURA CCC Sumbawanga kwa kusimama nasi wananchi wa mtaa wa Anglikani "A" tangia mwanzo wa lalamiko mpaka mwisho na katuongoza kwa kutupatia elimu kuhusu namna sahihi za kuwasilisha malalamiko yetu," alishukuru Bi. Adelina.

Bi. Adelina aliendelea kusema

kuwa bila elimu na msisitizo kutoka EWURA CCC kwa kuwakumbusha kuitambua haki zao kama watumiaji basi ni dhahiri wangeipoteza haki yao ya msingi ya kufidiwa kwa hasara walivyopata.

Kwa upande wake bwana Aswile Akilimali ambaye pia ni mkazi wa Mtaa wa Anglikani "A" alieleza kuwa yeye ni mmoja wa waathirika wa hitilafu hiyo ya umeme ambapo mashine zake mbili za kukoboa mpunga ziliharibika huku akikiri kuwa tukio la kulipwa fidia litamfanya kurudi tena kuwa imara kiuuchumi kwani sasa ataendeleza kiwanda chake cha kukoboa mpunga. Akilimali alitoa shukrani zake za dhati kwa ofisi ya EWURA CCC Mkoa wa Rukwa kwa kuwasaidia katika upatikanaji wa haki na fidia hiyo.

"TANESCO wamenilipa kiasi cha shilingi 2,880,000 ikiwa ni fidia ya uharibifu wa mashine zangu. Naishukuru na kuipongeza EWURA CCC kwa kazi ya kututetea sisi watumiaji. Kwa mara ya kwanza nimelitumia Baraza na nimepata msaada katika lalamiko ambalo sikutegemea kulipwa fidia kutohana na hasara nilioipata," alieleza Bw. Akilimali.

Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja wa EWURA CCC mkoani Rukwa Bw. Ramadhan Kakende ambaye ndiye aliyewasimamia wananchi hao katika hatua zote za kutatua lalamiko lao aliwataka watumiaji wote wa huduma za nishati na maji kuitumia EWURA CCC kama chombo chao cha utetezi.

"Nitoe wito kwa watumiaji wote wa huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA kuendelea kuitumia ofisi ya EWURA CCC katika kutatua changamoto zao wanazozipata katika kutumia huduma hizo kwani tutahakikisha haki zenu mnazipata kama wenzetu hawa waliopata leo. Jambo la muhimu ni watumiaji tusiha hau kutimiza wajibu wetu pia kwenye matumizi ya huduma hizi," alisema Bw. Kakende.

Aidha Bwana Kakende aliwasisitiza watumiaji kuwa EWURA CCC ni chombo chenye jukumu la kutetea na kuwawakilisha watumiaji wa huduma za nishati na maji hivyo basi waitumie pale wanapopata changamoto huku akiwaomba watumiaji kuwa wavumilivu pindi wanapotafuta haki zao kwani lalamiko hupitia hatua mbalimbali ikiwemo vikao vya usuluhishi mpaka hatua za uamuzi.

Tunaomba maji Maweni

Na Neema Nnko, Manyara

Wakazi wa kijiji cha Maweni-Galapo kilichoopo nje kidogo na mji wa Babati hivi karibuni wameilalamikia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati (BAWASA) kwa kutowafikishia mtandao wa huduma ya maji katika kijiji hicho.

Malalamiko hayo yametolewa na wananchi hao wakati Ofisi ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoa wa Manyara ilipokuwa ikitoa elimu kwenye kikao cha wananchi kilichoandaliwa na ofisi ya Serikali ya kijiji cha Maweni.

Wakizungumza kwa uchungu wananchi hao walieleza adha ambazo wamekuwa wakipitia kwenye huduma za maji ikiwemo kutumia gharama kubwa kupata maji, kutumia maji yasiyo salama kwa afya zao pamoja na uwepo wa ahadi wanazopewa na viongozi hasa wakati wa uchaguzi ambazo hazijazaa matunda hadi leo.

"Ni maombi yetu ya muda mrefu kupatiwa huduma ya maji ndani ya kijiji chetu. Tunatumia gharama kubwa kupata maji kutoka Galapo mjini na wakati mwagine maji haya yanakuwa siyo safi na salama kutokana na namna tunavyosa-

firisha," alisema Abdi Juma mkazi wa kijiji hicho.

Naye Bi. Wema Lotu alisema kuwa kijiji chao kimekuwa kikilalamikia kero hiyo ya kutokuwa na mtandao wa huduma ya maji kwa viongozi mbalimbali amba walishawahi kutembelea kijijini hapo, lakini hata hivyo bado changamoto hiyo hajatataliwa.

Wema alisema "asanteni kwa kuj



Tumekusudia

kupeleka maji Maweni na kata nzima ya Quash na hadi sasa tumeshafanya utaratibu wa kupata mabomba ya kutosha kifika kijijini hapo ambapo ni umbali wa kilomita 20. Ombi letu kwa wananchi wa eneo hili ni ushiriki wao wa nguvu kazi ili kuharakisha kazi hii na hatimaye wananchi wapate huduma ya maji," alisema Mha. Msuya.

Ofisi ya EWURA CCC Manyara imeendelea kutetea na kusimamia maslahi ya watumiaji kwa kuzingatia kanuni na taratibu kama lilivyo jukumu lake kuhanakisha huduma bora inawafikia watumiaji wote wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA ikiwa ni pamoja na kufuatilia utatuvi wa changamoto zinazowakabili.

kusikiliza na kuweka nia ya kutatua kero yetu ya maji. Tumekuwa tunapokea ahadi nyingi sana kuhusu kupatiwa maji hasa wakati wa uchaguzi ila hazijawahi kutekelezwa. Sisi kama wananchi wa hapa tupo tayari kutoa ushirikiano hata kwa nguvukazi zetu kuhakikisha huduma hii inatufikia ili kuondokana na adha hii."

Ofisi ya Baraza Mkao wa Manyara iliyasilisha kero hii kwa Mkurugenzi Mtendaji wa BAWASA Mhandisi Idd Msuya ambaye alieleza mipango na mikakati ya kufikisha maji kijijini Maweni ndani ya miezi michache ijayo.

"Tumekusudia kupeleka maji Maweni na kata nzima ya Quash na hadi sasa tumeshafanya utaratibu wa kupata mabomba ya kutosha kifika kijijini hapo ambapo ni umbali wa kilomita 20. Ombi letu kwa wananchi wa eneo hili ni ushiriki wao wa nguvu kazi ili kuharakisha kazi hii na hatimaye wananchi wapate huduma ya maji," alisema Mha. Msuya.

Ofisi ya EWURA CCC Manyara imeendelea kutetea na kusimamia maslahi ya watumiaji kwa kuzingatia kanuni na taratibu kama lilivyo jukumu lake kuhanakisha huduma bora inawafikia watumiaji wote wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA ikiwa ni pamoja na kufuatilia utatuvi wa changamoto zinazowakabili.

Changamoto

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA GEITA.

GEUWASA

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita inatekeleza Mradi wa Maji Wilayani Mbogwe wenye thamani ya Shilingi Milioni 822 amba unahusisha; Ujenzi wa tenki lenye ujazo wa lita 100,000, ujenzi

wa Nyumba ya pampu katika Chanzo cha Maji pamoja na ulazaji wa bomba kutoka katika Chanzo cha Maji mpaka lilipo Tenki.

Wasiliana Nasi Bure 0800 750 060

Geuwasa

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA JIJI LA ARUSHA

AUWSA

BILI YA MWEZI OKTOBA IMETOKA
Timiza wajibu wako kwa kulipa kwa wakati

LIPIA SASA
KWA HUDUMA BORA NA ENDELEVU.
"Mteja Wetu, Fahari Yetu."

Unaweza Kulipia Ankara (bili) yako Kupitia benki na mitandao ya simu.

C&B BANK NMB
TANZANIA TpBank
vodafone m-pesa tigo pesa
halopesa airtel money

Huduma Kwa Wateja Whatsapp
0800110069 0734 200 288

Mitandao ya Kijamii
@auwsatz



Bi. Bibie Mssumi, Afisa wa Elimu kwa Umma TAKUKURU Kinondoni, akitoa elimu juu ya masuala ya rushwa kwa wafanyakazi wa EWURA CCC wakati wa kikao cha wafanyakazi kilichofanyika Bagamoyo mkoani Pwani. Picha na Anadorice Komba

Baraza lafundwa kuhusu rushwa

Na Anadorice Komba, Kagera

Wafanyakazi wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) wameaswa kujiepusha na vitendo ya rushwa na mambo mengine yanayokiuuka madili ya kazi zao wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

Akizungumza wakati wa Kikao cha Nne cha Mwaka cha Wafanyakazi wa Baraza kilichofanyika Agosti 23, 2023 wilayani Bagamoyo, Kaimu Katibu Mtendaji wa EWURA CCC Bi. Stella Lupimo aliwaambia wafanyakazi wa Baraza kuwa masuala ya kupambana na rushwa ni moja ya lengo ambalo Baraza limeweka katika Mpango kazi wake wa mwaka 2023/24 ikiwa ni takwa la Serikali kuwa wafanyakazi katika taasisi za umma waelimishwe na kukumbushwa juu ya masuala ya rushwa.

Bi. Lupimo alisisitiza kwa kusema "naamini baada ya mkutano huu tutakaporudi katika vituo vyetu vya kazi tutafanya kazi zetu kulingana na kanuni na sheria na kuepukana na masuala ya rushwa mahala pa kazi."

Bi. Lupimo aliwaomba wafanyakazi wa Baraza hilo kwenda kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na maadili katika utandeji wao wa kazi huku akiwaasa kujiepusha na vitendo

ya rushwa ambavyo kwa namna moja au nyingine vinaweza kuchafua taswira ya taasisi au mfanyakazi kujikuta matatani.

Kwa upande wake mtoe mada kutoka ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Bi. Bibie Mssumi, alisisitiza wafanyakazi wa Baraza kutokujilingiza kwenye vitendo ya rushwa kwani kwa kufanya hivyo

“
**Serikali
inapambana
na rushwa** kwa
sababu rushwa ni
adui na kikwazo
cha maendeleo ya
Watanzania, hivyo
aliwaomba watumishi
wa EWURA CCC
kuhakikisha kuwa
wanafanyakazi katika
mazingira ambayo
hayatokaribisha
vitendo ya rushwa

itawafanya washindwe kuwatendea haki wananchi wanaowatumikia.

Bi. Mssumi alisema kuwa miongoni mwa vyanzo vinavyo chochea kuongezeka kwa vitendo vya rushwa ni pamoja na elimu ndogo kuhusu uraia na uzalendo na wananchi kutaka huduma kwa haraka. Sababu zingine ni adhabu ndogo kwa wala rushwa, upendeleo kwenye mfumo wa utoaji haki, huduma chache kwa jamii, fursa chache za kiuchumi, tamaa, ubinafisi na mifumo ya kodi isiyo rafiki.

Bi. Mssumi aliendelea kusema kuwa Serikali inapambana na rushwa kwa sababu rushwa ni adui na kikwazo cha maendeleo ya Watanzania, hivyo aliwaomba watumishi wa EWURA CCC kuhakikisha kuwa wanafanyakazi katika mazingira ambayo hayatokaribisha vitendo ya rushwa.

"Ili kufanikiwa kwenye vita dhidi ya rushwa hatuna budi kubadilisha mitazamo yetu ili tuwe ni watu wenye maadili na tunaochukia rushwa," alisema Bi. Mssumi.

Aidha aliwataka watumishi hao kuwaelimisha na kuwakumbusha watumiaji wa huduma za nishati na maji katika mikoa yao juu ya umuhimu wa wananchi kuepuka vitendo ya rushwa kwani vinazorotesha utoaji wa huduma kwa usawa na haki hasa katika sektora za nishati na maji.

Aliwaomba Maafisa kutoka EWURA CCC kuwahamasisha wananchi kutoa taarifa juu ya watoa huduma watakaoonesha kutaka rushwa ili kuwapatia huduma, kwani hii itasaidia kuboresha utoaji huduma na kudhibiti vitendo hivyo ya rushwa nchini.

Akitoa neno la shukrani kwa mtoe mada kwa niaba ya watumishi wa Baraza, Wadi Omari, Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala EWURA CCC Mkoa wa Geita, alimshukuru Bi. Mssumi kwa elimu hiyo aliyotoa yenyehengelo la kuimarisha maadili kwa watumishi katika kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

"Elimu hii itakuwa chachu ya mabadiliko kwa sababu mabadiliko yakanza na kila mmoja wetu basi itafuatia familia na mwisho wa siku jamii yote itabadi. Tunawaomba TAKUKURU kuendelea kutoa elimu hii kwa watumishi wa taasisi zingine na jamii kwa ujumla ili kujifunza madhara ya rushwa na hatimaye kubadili mienendo ya watumishi na jamii kwa ujumla na kuepuka madhara yatokanayo na rushwa," alisema Bw. Omari.

Maswali yaulizwayo mara kwa mara

Maswali na Majibu

Nini hupelekea mteja kukadiriwa anka-ra ya maji?

Mazingira yafuatayo hupelekea mteja kukadiriwa ankara ya maji kama ilivyo katika Kanuni za Ubora wa Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira za mwaka 2020, GN No. 849 vifungu namba 42(2) na 48(5).

- i. Mita ya mteja kuwa mbovu.
- ii. Mita kutofikika kwa urahisi (kuwa ndani ya uzio)
- iii. Endapo mita ya mteja haikuweza kusomwa na Mamlaka husika.

Je, mteja anaweza kukadiriwa matumizi ya umeme?

Sehemu B (1)(a) ya Mkataba wa Huduma kwa Wateja TANESCO inasema kuwa:-

- Wateja wote wanaotumia mita za malipo baada ya matumizi, mita zao zitasomwa angalau mara moja ndani ya miezi miwili (2).
- Kama mita haitasomwa katika mwezi wowote, matumizi ya mwezi huo yatakadiriwa na marekebisho kama yapo yatafanywa wakati mita itakaposomwa mwezi unaofuata.
- Wateja wanahimizwa kutoa taarifa kama mita hajasomwa kwa muda wa miezi miwili (2) mfululizo.

Na sehemu B (3) ya Mkataba huo inasema kuwa "kama italazimika kukadiria matumizi ya umeme katika kipindi fulani, msingi wa ukadiriaji utakuwa ni usomaji wa mita wa matumizi ya miezi mitatu ya nyuma."

Je, kuna fidia ya kucheleweshewa maunganisho ya huduma za maji nikiwa nimetimiza wajibu wangu wote?

Kanuni namba 54 (1) (b) ya Kanuni za Ubora wa Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira za mwaka 2020, Mtohuduma anapaswa kumu-

unganishia mteja mpya huduma ya maji ndani ya siku 7 za kazi baada ya malipo kufanyika.

Endapo hilo halikufanyika, kanuni hiyo imetaja fidia ya malipo ya Tsh 15,000 kama fidia ya msingi, na Tsh 5,000, kwa kila siku inayoongezeka bila kupatiwa huduma.

Ni nani mwenye jukumu la kuhakiki ufanisi wa mita ya maji kabla ya kuunganisha kwa mteja?

Kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Vipimo Sura 340 ya mwaka 2019, na Kanuni ya 46(1) ya Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira (Ubora wa huduma na leseni) za mwaka 2020; GN Na. 849 mwenye jukumu na wajibu wa kuhakikisha uthabiti na ufanisi wa mita ya maji ni Wakala wa Vipimo (WMA).

Hivyo ikiwa una mashaka na ufanisi wa mita yako ya maji, wasiliana na mtohuduma wako ili mshirikiane kupeleka mita hiyo ikapimwe na Wakala wa Vipimo.

Je, ni wakati gani Mamlaka ya Maji hairuhusiwi kusitisha huduma kwa mteja mwenye deni la maji?

Hairuhusiwi kusitisha huduma siku ya Ijumaa mchana, Jumamosi, Jumapili na siku za mapumziko (public holiday).

Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 57 (3) (c) (d) (e) ya Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira (Ubora wa huduma na leseni) za mwaka 2020; Tangazo la Serikali Na. 849.

Kwa nini baadhi ya vituo vya mafuta vinauza mafuta bila kuwa na mabango ya bei?

Kanuni ya 45(1) ya Kanuni za Mafuta za mwaka 2022, Tangazo la

Maswali yaulizwayo mara kwa mara

Serikali Na.150 inavitaka vituo vyote vya mafuta kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango (billboard) yanayoonekana bayana yakionesha bei ya mafuta, punguzo na vivutio vya biashara (promosheni) zinazotolewa na kituo husika. Kutokuweka bango ni kuvunja Kanuni hizi.

Nini utaratibu na gharama za maunganisho ya mita za umeme zaidi ya moja ndani ya nyumba moja?

1. Kwa mujibu wa Agizo la marekebisho ya bei ya umeme ya mwaka 2020, Gazeti No. 1020, gharama za maunganisho mapya ndani ya mita thelathini (30) toka miundombinu ya umeme ilipo ni shilingi za kitanzania 320,960 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa mjini na kwa vijiji itakuwa ni 27,000 kwa kila maunganisho mapya ya mita ya umeme.


2. Maunganisho ya mita zaidi ya moja ndani ya nyumba moja tafsiri yake ni maunganisho mapya ndani ya mita thelathini (30) ambapo gha-

rama yake ni shilingi za kitanzania 320,960. Utaratibu wake kulingana na mkataba wa huduma kwa wateja wa TANESCO ni mteja kujaza fomu ya kuomba huduma ya kuungiwa umeme na kuwasilisha viambatanisho vyote muhimu vinavyotakiwa ikiwemo picha moja na mchoro unaoonyesha nyaya zilizosambazwa kwenye jengo husika uliosainiwa na kupigwa muhuri na mkandarasi wa umeme aliyesajiliwa.

Ni kwa nini bei za mafuta zimekuwa zikibadilika mara kwa mara?

1. Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166, bei za bidhaa ya mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko, na EWURA itaendelea kuhamisisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa ya mafuta.

2. Hivyo bei za mafuta nchini hubadilika kulingana na bei katika soko la dunia kwa kuzingatia kanuni za kukokotoa bei za mafuta kama zilivyoainishwa kwenye Jedwali la



Maswali yaulizwayo mara kwa mara

Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za Bidhaa za Mafuta (zilizorekebishwa mwaka 2023) zikisomwa pamoja na Kanuni za Upangaji Bei za Bidhaa za Mafuta za mwaka 2022.

Je, nitajuaje usahihi wa bili ya maji nyumbani kwangu?

Kanuni ya 42(1) ya Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira (Ubora wa huduma na leseni) za mwaka 2020; GN Na. 849 inaelekeza kuwa ni lazima Mto huduma asome mita ya mteja kabla ya kuandaa bili yake ili kujua kiwango halisi cha maji kilichotumiwa na mteja kwa mwezi husika.

Hivyo ili kujua usahihi wa bili yako ni lazima uhakikishe kuwa mita yako ya maji inasomwa kila mwezi na ujiridhishe na usomaji huo kama uko sahihi.

Nini wajibu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) kwa wateja wake?

Pamoja na wajibu mwingine, MUWASA katika Mkataba wake wa huduma kwa wateja toleo la No 1 2020, inakiri yafuatayo kuhusu wajibu wake kwa mteja:-

- Kutoa huduma bila upendeleo wala itikadi za kisiasa.
- Kuheshimu utawala wa kisheria, kutoa huduma bila kukiuka sera, sheria, kanuni, miongozo nyaraka na taratibu zilizopo.
- Kuwa na mahusiano bora na wateja.
- Kutoa huduma bora zinazokubalika na viwango bora.

Ni utaratibu upi unatumika kum-rejeshea mteja wa TANESCO ambaye amechania ujenzi wa njia ya kusambazia umeme ili kupeleka umeme nyumbani kwake mbali na gharama za laini ya huduma?

Mteja wa umeme aliyeomba huduma na kuchangia ujenzi wa njia ya usambazaji wa umeme nje ya laini ya huduma (service line), wakati TANESCO haina bajeti ya kupeleka umeme katika eneo hilo atarudishiwa fedha zake kwa kupewa punguzo la 40% kuititia manunu ya umeme kwa mwezi hadi gharama alizotumia zitakapo kamilika kulipwa

Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Umeme ya mwaka 2008, pamoja na Mwongozo wa Wahandisi wa TANESCO wa mwaka 2014.

Ni mahali gani sahihi pa kutoa taarifa ya uharibifu wa miundombinu ya maji?

Taarifa za uharibifu wa miundombinu ya maji zinapaswa kupeleka kwenye ofisi za mto huduma au mamlaka zingine za kisheria.

Sheria ya Maji Na. 5 ya mwaka 2019 kifungu cha 61 inabainisha faini au kifungo cha miaka isiyopungua 2 na isiyozidi 5 au faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki 5 na kisichozidi milioni 5 kwa mtu yeoyote atakayethibitika kuharibu miundombinu ya maji.

Je, ni kwa namna gani EWURA CCC imejipanga kutoa elimu kwa jamii?

EWURA CCC hutoa elimu kuhusu huduma za nishati na maji kwa makundi mbalimbali ya watumiaji kwa mujibu wa Sheria ya EWURA Sura 414 kifungu cha 31(1) (a-b). Pamoja na masuala mengine,

Maswali na Majibu

Maswali na Majibu

Maswali yaulizwayo mara kwa mara

EWURA CCC hutoa elimu kwa makundi mbalimbali ya watumiaji kuhusu haki na wajibu wao.

Je, kuna għarama za "survey" kwa mteja mpya anayeomba kuunganishwa na huduma za maji?

Hakuna għarama zozote kwa ajili ya "survey." Rejea ya 37(3) na Jedwali 4 la Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, 2020, GN. No. 849.

Je, mteja anawexa kuhoji kwa TANESCO kuhusu utimamu wa mita ya umeme?

Ndio. Sehemu B(2)(a-e) ya Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa TANESCO inaeleza utaratibu wa kufanya uchunguzi wa mita ya mteja na kwamba mteja ana haki ya kuhoji usahihha wa mita za matumizi ya kabla ya malipo au mita za matumizi baada ya malipo.

Ni maji yapi bora na salama?

Kwa mujibu wa tovuti ya Wizara ya Maji Tanzania <https://www.maji.go.tz/faqs> inaelezwa kuwa ni maji yeyote yale ambayo yamehaki-kiwa ubora wake kifizikia, kikemia na kibaolojia na kukidhi viwango vinavyokubalika kwa matumizi na usalama wa mlaji (mwananchi) na hayana athari za kiafya.

Tufanye nini sisi wapangaji pale ambapo wamiliki wa nyumba tulizopanga wanapotutoza bei kubwa ya umeme tofauti na ile ya TANESCO?

Kanuni ya 14 ya Kauni za Umeme za Jumla, 2020 zinaeleza kuwa mamiliki wa nyumba anawexa kufunga mita ndogondogo ili kupima matumizi ya kila mpangaji na kulipa għarama ile ile ambayo Shirika linatoza.

Hakuna anayeruhusiwa kuuza umeme bila kibali cha Mamlaka zinazohusika. Aidha wateja wana-shauriwa kuhakikisha maswala yote ya malipo ya umeme au endapo kutakuwa na deni yaingizwe kwenye mkataba wa pango ili kuondoa sintofahamu ambayo inaweza kujitokeza baadaye.



Maswali ya ulizwayo mara kwa mara

Maswali na Majibu

Nini kifanyike kwa mtumiaji anayepaswa kulipwa fidia baada ya kupata huduma mbovu ya umeme?

Kanuni za Usambazaji ya Huduma za Umeme 2019, tangazo la Serikali No. 387 kifungu 23(2)(3) inasema mtu ye yote aliyeathirika kwa kuumia, kupoteza maisha au mali kutokana na usambazaji wa huduma ya umeme anatakiwa kupeleka malalamiko yake kwa mtohuduma kwa ajili ya utatuzi.

Kama malalamiko hayo yatashindwa kutatuliwa basi yawasilishwe kwa Mamlaka ya Udhhibit ya Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwa ajili ya kushughulikiwa kisheria.

Je, kuna gharama zipi ninapohitaji kuchukua fomu ya kuunganishiwa huduma ya maji?

Kanuni ya 37(1) ya Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, 2020, tangazo la Serikali No. 849 inaeleza kwamba mteja atatuma maombi kwa mtohuduma kwa ajili ya kuunganishiwa na huduma. Fomu hizi hutolewa pasipo malipo yotote.

Je nifanye nini endapo nimelipa ankara ya maji nikakosea namba ya malipo (control number)?

Hatua za kuchukua:

- Fika ofisi za Mamlaka ya maji ukiwa na meseji ya malipo (kama malipo uliyofanya kwa simu) au risiti ya malipo (kama ulilipa kwa benki) uliyofanya.
- Kama huna meseji ya malipo ya simu basi tembelea ofisi za mtandao wa simu husika uombe historia

ya miamala uliyofanya (statement) kisha iwasilishe ofisi za Mamlaka ya maji kwa ushughulikiaji.

Ni muhimu kwa watumiaji ku-hakiki namba ya akaunti na namba za malipo kabla ya kufanya malipo.

Je nifanye ikitokea nimefuta bili niliyotumiwa ya maji au meseji ya Luku nilizonunua?

Mteja anaweza kupakua ap-likesheni ya GePG na kisha kuchagua huduma ya maji au umeme na kufuat-ka maelekezo ili kuweza kupata

- Bili ya maji
- Kupata maelezo ya luku ya mwisho uliyonunua
- Kufanya malipo ya huduma za nishati au maji

Mteja anaweza kupiga simu au kufika ofisi za Mamlaka ya Maji au TANESCO kwa msaada zaidi.

Je ni adhabu gani hutolewa endapo Mamlaka ya maji itasitisha huduma kwa mteja kimakosa?

Ikithibitika kuwa Mamlaka imesitisha huduma kimakosa basi itapas-wa kurejesha huduma hiyo ndani ya masaa 24. Kushindwa kufanya hivyo mtohuduma atalazimika kumfidia mteja fedha taslimu. Rejea Kanuni ya 58 na Jedwali No. 3 la Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira (Ubora wa huduma na Leseni) Mwaka 2020 Tangazo la Serikali namba 849.

Je ni kwa nini bei za mafuta hutofauti-na kutoka kituo kimoja hadi kingine ilihali mafuta ni yaleyale?

Kwa mujibu wa Kanuni za EWURA za Upangaji wa bei za mafuta za

Maswali na Majibu

Maswali yaulizwayo mara kwa mara

mwaka 2022,

Kanuni ya 4 (1), (2), (3) na (4) vituo vya mafuta vimepewa uhuru wa kuza bidhaa za mafuta ya petrol kwa bei ya ushindani lakini hawat-akiwi kuvuka bei kikomo (price cap) ambayo imewekwa na EWURA kwa kipindi kilichotangazwa.

Uhakiki na ukaguzi wa mizani za kupimia ujazo wa gesi (LPG) huwa unafanywa mara ngapi kwa mwaka kwa wauzaji wa gesi?

Kanuni ya 3 na ya 4 ya Kanuni za Wakala wa Vipimo za mwaka 2019 shughuli ya uhakiki na ukaguzi wa mizani za kupimia ujazo wa gesi ya LPG hufanywa kila mara, na angalau mara moja kwa mwaka. Ukaguzi huu hufanywa kwa wauzaji wote wa mitungi ya gesi ya matumizi ya majumbani.

Taratibu zippi zinatumika kuomba huduma mpya ya maji kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira GEUWASA?

Kipenge Na. 6.1.1 cha Maktaba wa Huduma kwa Wateja GEUWASA

kinaeleza hatua za kufuata ili kupata huduma ya maji kama ifuatavyo:-

- Mteja napaswa kufika Ofisi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Geita au kutembelea Tovuti yake ya <https://www.geuwsa.go.tz/> kwa ajili ya kufanya maombi ya huduma ya maji na kuijandikisha.
- Fomu zinapatikana Ofisi ya Huduma kwa Mteja bila malipo yoyote na Mteja atalazimika kuja na picha 2 ndogo za rangi (passport) pamoja na nakala ya kitambulisho cha Mpiga kura au Uraia au Leseni ya udereva au Barua toka Serikali ya mtaa.
- Baada ya kuijandikisha Watalamu wa Mamlaka watafanya ukaguzi (survey) kwenye eneo/nyumba inayoombevu huduma ya maji na kutayarisha gharama ndani ya siku 2 za kazi.
- Mteja atapata taarifa ya ukaguzi na gharama za kuungwa maji ndani ya siku 4 kuanzia tarehe aliyo-fanya maombi ya huduma ya majisafi.



Maswali yaulizwayo mara kwa mara

Maswali na Majibu

- Taarifa hizi atazipata kwenye ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Geita.

Je, gesi ya kupikia majumbani inaweza kuchakachuliwa?

Ndio. Gesi inaweza kuchakachuliwa hasa kwenye kupunguza uzito kwenye mitungi.

Hata hivyo ni kosa kisheria kuja za au kurudia kujaza gesi ya kupikia majumbani tofauti na maeneo am-bayo yameidhinishwa kwani kufanya hivyo ni kosa kwa mujibu wa Kanuni ya Mafuta (LPG Operations) kifungu cha 32. Kwa atakayebainika kufanya hivyo atakuwa amevunja Kanuni 32 (1) na adhabu yake ni kwenda jela si chini ya miaka 3.

Nifanye nini endapo nitasitishiwa hudumza ya maji kwa madai ya deni wakati nina mkataba na mtoa huduma wa kulipa deni langu kwa awamu?

Toa taarifa kwa mtoa huduma na wasilisha ushahidi wote kuthibitisha malalamiko yako ikiwemo nakala ya

mkataba wa kulipa kwa awamu.

Kama hutaridhishwa na nam-na mtoa huduma alivyoshughulikia malalamiko yako wasilisha malalamiko hayo EWURA.

Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 4(1) na (2) ya Kanuni za Utatuzi wa Malalamiko za mwaka 2020.

Nini wajibu wa TANESCO inapomkatia mteja huduma kimakosa kwa madai ya kuto-lipia matumizi? Kifungu cha 5(h) cha

Mkataba wa huduma huduma kwa wateja wa TANESCO kinasema endapo TANESCO itamkatia umeme mteja kimakosa kwa madai ya kuto-lipia matumizi basi TANESCO itawajibika kumfidia mteja husika kwa kiwango kilichowekwa kwenye Kanuni zilizotungwa na Mdhibiti (EWURA).

TANESCO itawajibika kumfidia mteja mara tano (5) ya kiwango cha bei ya umeme ya TANESCO kwa kiasi cha umeme ambacho mteja alikikosa kwa kuangalia matumizi ya mteja kwa siku thelathini (30) zilizopita.





Nukuu Maridhawa

“

Utatuzi wa kero za wananchi ni moja ya vipaumbele muhimu vya Baraza na katika kipindi hiki Baraza limepokea jumla ya malalamiko 1,946 kutoka kwa watumiaji ambapo kati ya malalamiko hayo, 1,011 yanahusu huduma za maji, 857 ni kuhusu umeme, 66 ni kuhusu mafuta, na 12 ni kuhusu gesi ya LPG.

-- *Kaimu Katibu Mtendaji wa EWURA CCC,
Bi Stella Lupimo*

“

natambua wafanyakazi mnajitoa katika kutekeleza majukumu yenu na mnafanya kazi kwa ufanisi mkubwa lakini lazima tuongeze bidii ili malengo ya Baraza yaweze kufikiwa. Ni matarajio ya Baraza kuwa mtahitimisha kikao hiki kwa maazimio yatakayowapa nguvu ya kwenda kufanya kazi kwa bidii na uadilifu
-- *Mwenyekiti wa EWURA CCC,
Mhandisi David Ngula*